epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Ijumaa Novemba 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581854
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda

# Adaiwa kumlewesha mwanafunzi wake, akambaka darasani

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipatiwa ufafanuzi na SACP Daimu Mmolosha (kushoto) namna Gereza la Isanga lilivyotii agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuzitaka taasisi zote za serikali zinazohudumia zaidi ya watu 100 kutumia nishati safi kupika alipozuru gerezani huko jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

UK. 21



## NEYMAR KUTIBIWA WIKI NNE HADI SITA

## Rais Samia amhakikishia Trump kumpa ushirikiano



UKURASA 3

UKURASA WA 2

## MPINA AREJEA BUNGENI AKIWA NA HOJA 5 NZITO



MBUNGE wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina amemaliza adhabu yake ya...

UKURASA WA 3

UTEUZI WAGOMBEA LEO

## CHADEMA, ACT WATOA ANGALIZO, MSIMAMIZI WA UCHAGUZI ANG'AKA

WAKATI majina ya wateule wa kuwania nafasi mbalimbali katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu yanatarajiwa...

UKURASA WA 3

## AJALI YA HIACE, LORI ILIVYOWAUA WATU 14, TISA WAJERUHIWA

WATU 14, wakiwamo watoto wachanga wawili, wamefariki dunia papo hapo na wengine tisa kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha haice na fuso...



# Wahariri wampa waziri madai yao

UKURASA 4




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Mpina arejea bungeni akiwa na hoja tano nzito

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina amemaliza adhabu yake ya kutohudhuria vikao 15 bungeni, akiwa na hoja tano, ikiwamo kutaka mkataba kati ya serikali na kampuni ya DP World uwasilishwe bungeni.

Vilevile, mbunge huyo ameandaa maoni kuhusu masuala ya kodi yenye kurasa 50 ili kuyawasilisha kwa Tume ya Maboresho ya Mifumo ya Kikodi.

Hoja zingine zinazohusiana na utekelezaji mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG), kutokamilika kwa wakati Mradi wa Bwawa la Uzalishaji wa Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) na utaratibu wa usafirishaji mizigo uliosababisha wafanyabiashara kukosa nyaraka.

Akichangia bungeni jana mjadala wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2025/26, Mpina alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunda tume hiyo na kwamba pamoja na kuwa alikuwa "mapumziko", ameandaa kurasa 50 atakazowasilisha kwa tume hiyo namna nchi inavyopoteza mapato.

"Kwa muda mrefu tumeongelea hili bungeni, ninaamini matokeo ya hiyo tume yataleta mageuzi makubwa sana katika ukusanyaji mapato nchini. Hongera sana Rais kwa kuliona hili.

"Na mimi kwa kulichukulia uzito jambo hili, pamoja na kuwa nilikuwa mapumzikoni, tayari nimeandaa kurasa 50, nitapeleka tume, kurasa zimezungumzia maeneo mbalimbali nchi inavyopoteza mapato," alisema.

Mpina, akizungumzia suala la mkataba wa DP World na serikali, alisema walikubaliana mikataba ya aina hiyo kupelekwa bungeni na kwamba ilielezwa mwekezaji atawekeza Dola milioni 250 kwa miaka mitano na kudai kuwa mwekezaji huo ameanza kukusanya kodi.

"Tulikubaliana hapa bungeni mikataba hii mikubwa, yote mitatu, italetwa kwenye hili Bunge ili tujue kilichokubalika ndani ya mikataba hiyo, lakini Sheria yetu ya Rasilimali za Asili inasema mikataba yote ya rasilimali iletwe bungeni, ninaendelea kuuliza hivi imeshindikana nini kuleta mikataba ya Bandari ya Dar es Salaam tuliyoingia na DP World bungeni?" Mpina alihoji.

Kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mbunge Mpina alisema mradi huo tayari uzalishaji umeanza na megawati 740, lakini haijulikani huo mradi unakamilika lini ili kupata megawati zote 2,115.

"Tuliwaahidi wananchi kwamba umeme huu ni umeme wa bei nafuu, hatujaambiwa kwenye mpango huu unafuu wa mradi, tuliahidi kushusha umeme kwa wananchi wetu, na hatujaambiwa ni nchi ngapi tumeingia nazo mkataba wa kuziuzia umeme, na umeme utashuka kwa gharama kiasi gani ili wapate wananchi na wawekezaji kwa bei nafuu," alisema.

Mpina alisema kuwa katika mradi wa LNG, mazungumzo yamekuwa ya muda mrefu na kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Ralisimali za Asili, mikataba ya aina hiyo inapaswa kupelekwa bungeni na kuhoji mazungumzo hayo yatakuwa ya muda gani kwa kuwa inatakiwa utekelezaji wa mradi uanze kwa haraka ili nchi inufaike.

Mbunge huyo alisema kuwa katika mkataba wa usafirishaji mizigo wa kuchangia makasha kwa wasafirishaji mizigo tofauti, sheria ya usafirishaji huo ilibadilishwa sambamba na kanuni zake.

"Ilifika mahali msafirishaji wa mizigo anasafirisha na majina ya nyaraka zote yanaandikwa kwa jina lake, lakini tukapata matatizo ya wafanyabiashara wengi kukosa nyaraka za ulipaji kodi kwa sababu majina yameandikwa ya msafirishaji, mwisho wa siku wananchi wakashindwa kuuza bidhaa kwa kutoa risiti na wakashindwa kutumia EFD na migomo ikatokea kule Kariakoo," alisema.

Alisema hali hiyo imesababisha fedha nyingi kupotea na kushauri kampuni (jina tunalo) ambayo kwa miaka mitano imefanya kazi hiyo na inapofika kwenye kutoa mizigo nyaraka hazionekani.

"Naomba ufanyike ukaguzi wa kiuchunguzi kuchunguza kampuni ya... (alitaja jina la kampuni) kwa miaka mitano ili kubaini kodi iliyopotea ili kampuni ilipe hasara hiyo kwa serikali," alisema.

Hapo Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliomba kuzungumzia mkataba wa bandari ambao Mpina anataka upelekwe bungeni, akidai hakuna kodi yoyote inaruhusiwa kukusanywa na taasisi yoyote isiyo ya serikali.

"Na kwa mantiki, alilokuwa analiongelea la DP World, hakuna kodi yoyote DP World wanakusanya. Kodi zote ambazo zinakusanywa bandarini, zikiwapo import duty, excise duty, VAT, kodi ya reli, zote... custom processing fee, zote zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Na kimsingi, baada ya DP World kuanza shughuli zile ambazo zimeongeza ufanisi bandarini, kodi inayokusanywa na TRA imeongezeka na kufikia Sh. trilioni 1.23, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tangu TRA ianzishwe," alisema waziri huyo.

Waziri Mwiguli aliendelea kusema, "Kwa maana hiyo, kauli aliyotoa Mbunge wa Kisesa kwamba DP World wameanza kukusanya kodi ni ya uongo na imelenga kulipotosha Bunge na watanzania na kama hajafanya kwa makusudi, ninaomba afute kauli hiyo," alisema.

Akitoa majibu kuhusu hoja hiyo ya Waziri Mwigulu, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, alimwita Mpina, naye katika maelezo yake alisema: "Wakati ninachangia, kama nilitumia neno kodi, nilimaanisha tozo zinazokusanywa na DP World, sasa baada ya kuwa imekabidhiwa tangu Aprili 2024, kama nimetumia neno 'kodi DP World imekusanya', ninalifuta kwenye kumbukumbu sahihi za Bunge na mimi nilimaanisha tozo ambazo sasa hivi wanakusanya DP World."

Naibu Spika alielekeza kufutwa kwa maneno yanayoleta upotoshaji kwenye kumbukumbu za Bunge na kuwataka mawaziri kutolea ufafanuzi papo kwa papo wanapoona kuna jambo litasababisha ukakasi kwa umma.

Naye Mbunge wa Musoma Vijijini (CCM), Prof. Sospeter Muhongo alisema kuna fursa za ajira nje ya nchi na kuwataka Watanzania wasing'ang'anie kupata kazi nchini.

"Marekani wanataka wataalamu, Ulaya wameanzisha blue card, watahitaji watu, nchi kama Ujerumani inahitaji wataalamu wa sekta sita za masuala ya afya, uhandisi, ujenzi, kilimo, misitu na Ufaransa inahitaji wataalamu kwenye maeneo 23, sasa Watanzania tusing'ang'anie kazi nchini," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Kisesa, Luhaga Mpina, akichangia hoja ya mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka 2025/2026 na mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwalimu adaiwa kumlewesha mwanafunzi kisha kumbaka

**Na Restuta Damian,** MULEBA

MWALIMU wa taaluma katika Shule ya Msingi Rulanda, wilayani Muleba, mkoani Kagera, anatuhumiwa kumpaka na kumnywesha vitu vinavyodhaniwa kuwa dawa za kulevya, mhitimu wa darasa la saba aliyefika shuleni huko kufuatilia matokeo yake ya Mtihani wa Taifa mwaka huu kisha kumnajisi.

Akisimulia tukio hilo juzi nyumbani kwao, binti huyo mwenye umri wa miaka 13 (jina tunalo), alidai kuwa Oktoba 30 mwaka huu, saa tisa alasiri, alikwenda shuleni huko kufuatilia matokeo yake.

Alidai kuwa akiwa shuleni huko, alikutana na mwalimu huyo (jina tunalihifadhi) kwa lengo la kuangalia matokeo yake. Naye (mwalimu) alimweleza kuwa amepata Daraja "D".

Msichana huyo alidai kuwa baada ya kupewa matokeo yake, mwalimu huyo alimtaka arudi shuleni huko saa 10 jioni ili kumpatia ushauri kutokana na kuwa na matokeo yasiyoridhisha.

Alidai akiwa kwenye moja ya madarasa, alikokuwa anasoma baada ya kuitikia wito huo, mwalimu huyo alifika na kufunga mlango na madirisha na kumtaka avue nguo.

Mwanafunzi huyo alidai kuwa mwalimu huyo alimpaka vitu sehemu mbalimbali za mwili na baada ya hapo, akapoteza fahamu na alipozinduka, alimwona mwalimu akichungulia dirishani na kumtaka aondoke.

Mama wa mtoto huyo (jina tunalo) alidai kuwa ilipotimu saa 11 jioni siku hiyo pasi na kumwona mwanawe, alikwenda shuleni kumtafuta bila mafanikio.

Alidai kuwa ilitimu saa 1:30 jioni, mwanawe alirejea nyumbani na walipomhoji, alidai mwalimu wake alimfungia ndani na kumziba mdomo asipige kelele na kumpaka dawa.

Mama huyo alidai kuwa alipomchunguza mwanawe, alibaini alikuwa ameingiliwa kimwili kutokana na kuwa na michubuko sehemu za siri.

"Tulikwenda Kituo cha Polisi Muleba tukapewa PF3 (Fomu Na. 3 ya Polisi) kwa ajili ya kwenda hospitali kufanyiwa vipimo ndipo tulipompeleka Kituo cha Afya Kaigara kwa ajili ya huduma za kitabibu na baada ya hapo, tuliambiwa mtuhumiwa amekimbilia kusikojulikana," alidai.

Mama huyo aliendelea kueleza kuwa baada ya siku kadhaa, ndugu wa mwalimu huyo waliojitambulisha kama kaka na rafiki yake, walifika nyumbani kwake wakiomba suala hilo limalizwe kifamilia ili mtuhumiwa arejee kazini, lakini alikataa ombi hilo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Lameck Jonas, alikiri kuwa na taarifa za tukio hilo, akieleza kuwa alipokea simu ya Ofisa Mtendaji wa Kata kuwa mzazi wa mtoto ameripoti kuhusu mtoto wake kufanyiwa ukatili huo.

"Kwa taarifa ambazo nilipokea ni kwamba, siku ya tukio hilo, pikipiki ya mwalimu ilionekana mazingira ya shuleni na siku hiyo hakukuwa na programu ya kufundisha jioni kwa sababu madarasa ya mitihani yamekwisha," alisema.

Diwani wa Rulanda, Evance Ernest, alisema alipokea taarifa hiyo kutoka kwa Ofisa Elimu Kata kwamba, amepokea hati kutoka Jeshi la Polisi iliyopelekwa kwake baada ya wazazi wa mtoto kupewa PF3 kwa ajili ya matibabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Isaya Mbenja, alisema taarifa za ukatili huo amezipokea na katika maadili ya kazi, kuna tume ambayo husimamia nidhamu ya walimu.

Alisema halmashauri itaendelea na hatua ya kupelekwa taarifa za tuhuma hizo ili mamlaka zianze kufanya ufuatiliaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda, alitafutwa na Nipashe kwa njia ya simu kuzungumzia tukio hilo, akidai kuwa alikuwa nje ya ofisi kikazi. Aliahidi kuzungumzia suala hilo akiwa ofisini baada ya kupata taarifa kamili.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

## CHADEMA, ACT wadai kuna rafu uteuzi wagombea Serikali za Mitaa

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI majina ya wateule wa kuwania nafasi mbalimbali katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu yanatarajiwa kuwekwa hadharani leo, baadhi ya vyama vya upinzani vimeendelea kulia na rafu kwa wagombea wao.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema hakitakubali kuona wagombea wake wakienguliwa, huku ACT-Wazalendo kikidai kuwa na taarifa za wagombea wake kurubuniwa na wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Pwani, Boniface Jacob, alisema jana kuwa hawapo tayari kurudi nyumbani kufuta machozi 'kuomboleza' kwa wagombea wake kuenguliwa kwa sababu ambazo ni nje ya zile za kikatiba ambazo mgombea anatakiwa kuwa nazo.

"Safari hii hatususi, hatukimbii wala hatuliilii ovyo, hiari ni yao pawe na uchaguzi au pasiwe na uchaguzi. Kesho (leo) ni siku ya uteuzi, wanachama wetu, viongozi na wagombea tukusanyike tangu asubuhi kwenda kuangalia majina kama tumeteuliwa au hatujateuliwa. Kama hatujateuliwa tusirudi nyumbani.

"Tumtafute mteuaji tukamhoji, kwa lolote ambalo litakuwa limeandikwa katika ubao, ninyi nyote ni mashahidi, hakuna mgombea ambaye amejaza fomu peke yake, wote wamejaza chini ya wanasheria Kanda ya Pwani mpaka zinarudishwa," alisema.

Jacob pia aliwaonya wagombea wa chama hicho ambao wanapanga kufanya hujuma kwa kujitoa katika uchaguzi huo baada ya kuteuliwa, akisisitiza kuwa sababu pekee ya chama hicho kukosa mgombea ni kifo na si vinginevyo.

"Tumekupa nafasi kwa kukuheshimu na kukuona unatosha kugombea eneo hilo na wewe tuheshimu. Kila mtu ana tamaa, kila mtu ana njaa. Njaa zako funga breki. Kama ulichukua fomu ukataka kugombea, ukifikiri nafasi hiyo ni ya biashara, biashara hiyo ni ya hatari, acha!" Jacob alionya.

Msemaji wa ACT-Wazalendo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Rahma Mwita, alidai makada wa chama kimoja cha siasa nchini wanawalaghai wagombea wao ili wajiengue.

Alidai wanao ushahidi wa vitendo hivyo katika baadhi ya maeneo, yanayojumuisha Halmashauri za Tandahimba, Kondoa Mjini, Kondoa Vijijini, Kilwa, Chalinze, Kigoma Mjini na Nyamagana. Alisema kanuni zinazuia mgombea kujiondoa kabla ya uteuzi.

"Taarifa tunazozikusanya zinaonesha kuwa upo mpango wa wasimamizi wa uchaguzi kuzichafua au kuziongea taarifa fomu za kugombea, ili kuwapotezea sifa za kuteuliwa wagombea wa ACT Wazalendo na vyama vingine vya upinzani," alidai Mwita.

Alimtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kusimamia kanuni na taratibu za uchaguzi huo, ikiwamo vyama kuchagua ngazi ya kudhamini wagombea wake.

Alisema chama hicho kimejiandaa kushiriki uchaguzi na kimesimamisha wagombea wa kutosha waliowapa mafunzo ya namna ya kujaza fomu vizuri.

Naye Msimamizi wa Uchaguzi Jiji la Dodoma, Dk. Fredrick Sagamiko, amekanusha shutuma zinazoenezwa katika mitandao ya kijamii kuwa zipo njama za kuwaengua baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani katika uchaguzi huo.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini kuhusu shutuma hizo na mwenendo wa mchakato wa uchaguzi huo, akisisitiza hakuna taarifa yoyote ambayo imetolewa kuwa ni kiongozi wa chama gani ambaye amekosa sifa aliye na sifa ya kugombea katika uchaguzi huo.

Alisisitiza mchakato wa uchaguzi huo ni wa wazi, hivyo hakuna mkakati au nia yoyote ya kuminya demokrasia kwa baadhi ya vyama vya siasa.

***Imeandaliwa na Restuta James na Elizabeth Zaya (DAR) na Paul Mabeja (DODOMA)**

# Rais Samia amhakikishia Trump kumpa ushirikiano

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemwahidi Rais mteule wa Marekani, Donald Trump, kuendeleza ushirikiano na taifa hilo katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na wa kibiashara.

Kupitia ukurasa wa X, Rais Samia alimpongeza Trump kwa ushindi huo na kuahidi kuendeleza ushirikiano wa pamoja kati ya Tanzania na nchi hiyo kwa maendeleo ya wananchi wake.

"Kwa niaba ya serikali na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatuma pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Donald Trump, Rais Mteule wa Marekani kwa ushindi wako katika uchaguzi.

Mheshimiwa Rais Mteule, ninakutakia kheri. Ninatumaini kushirikiana nawe kuimarisha uhusiano baina ya Tanzania na Marekani," alimwahidi Trump.

Aidha, Rais wa Kenya, William Ruto, alisema nchi yake ipo tayari kuimarisha ushirikiano kwenye biashara, uwekezaji, teknolojia na ubunifu, amani na usalama na maendeleo endelevu.

Alisema nchi hiyo inathamini ushirikiano wao wa muda mrefu uliodumu kwa miaka 60 na kujengwa misingi, demokrasia, maendeleo na kuheshimiana.

Rais Ruto alisema anatarajia kuimarisha ushirikiano huo kwa kufanya kazi kwa pamoja kukabiliana na changamoto za kimataifa, kukuza amani na usalama na kuendeleza ukuaji wa uchumi shirikishi kwa manufaa ya wananchi.

"Kenya iko tayari kuimarisha ushirikiano wetu katika masuala ya maslahi ya pamoja kama biashara, uwekezaji, teknolojia na ubunifu, amani na usalama, na maendeleo endelevu," alisema.

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alisema anatarajia kushirikiana na Rais Trump kwa miaka ijayo kwa faida ya wananchi wa nchi hizo.

"Ujumbe wako umeweka wazi kuwa Marekani inapaswa kuwa mshirika wa uchaguzi unaovutia kwa mfano wake, badala ya kulazimisha mitazamo na njia zake za maisha kwa wengine," alisema.

Katika kinyang'anyiro cha urais wa Marekani, Trump alimshinda Kamala Harris, mgombea wa Democrat kwa kupata kura za wajumbe maalum 294, ambao ni 24 ya wajumbe 270 wanaotakiwa kupata ushindi.

Alimshinda majimbo muhimu kama Pennsylvania, Georgia, North Carolina na Wisconsin.

Wafuasi wake wanamchukulia Rais huyo mteule kutoka Chama cha Republican kama mwokozi na shujaa, aliyekuwa tayari kutetea maadili yao dhidi ya wanamageuzi nchini Marekani.



Mshtakiwa wa kesi ya mauaji ya mkewe na kisha kumchoma moto kwa magunia ya mkaa, Hamisi Luoga (kushoto), akiwa kizimbani huku akijadiliana jambo na mawakili wake, Mohamed Majaliwa (kulia), Zidadi Mikidadi (katikati) na Fatuma Abdul, baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wa shtaka linalomkabili katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Ajali ya Hiace, lori ilivyowaua watu 14, tisa wajeruhiwa

**Na Vitus Audax**

WATU 14, wakiwamo watoto wachanga wawili, wamefariki dunia papo hapo na wengine tisa kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha Haice na fuso katika kijiji cha Mwasengo, tarafa ya Mwakarungi, wilayani Nzega, mkoani Tabora.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana asubuhi, ikihusisha gari T 562 DGG aina ya Toyota Haice na lori T 361 CSB aina ya fuso.

Alisema ajali hiyo ilitokea baada ya dereva wa Haice kuligonga kwa nyuma roli hilo na kuingia chini ya uvungu wakati akitaka kulipita gari lingine akiwa katika mwendokasi.

"Ajali imesababisha vifo vya watu 14, wakiwamo watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja pamoja na majeruhi tisa ambao wanaendelea kupatiwa matibabu," alisema SACP Abwao.

Alisema majeruhi wawili wanaendelea kutibiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega, huku wengine saba wakipatiwa rufani kwenda Hospitali ya Rufani Nkinga, wilayani Igunga.

Alisema jeshi hilo linaendelea kumsaka dereva wa Haice ambaye alitokomea kusikojulikana baada ya kusababisha ajali hiyo, huku akiwataka madereva kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazosababisha madhara katika maisha ya watu.

Vilevile, aliwataka abiria wanaokuwa katika magari, wahakikishe wanapaza sauti, hasa pale wanapoona mwenendo mbaya wa uendeshaji wa dereva ambao haufuati sheria na kuhatarisha maisha yao.


**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA**

**COFFEE HUB COMPANY LIMITED**

**Cheti cha Usajili No. 138836932**

Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni COFFEE HUB COMPANY LIMITED, yenye usajili namba 138836932 kitakachofanyika tarehe 27/11/2024 ofisini kwa mfilisi saa 4:30 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi | **LINDA ALLAN MWAMBETE** |
| Amwani ya Mfilisi | **368 MSASANI ROAD<br>MIKUMI HOUSE<br>OYSTERBAY<br>P.O BOX 9673<br>DAR ES SALAAM<br>TANZANIA** |
| Tarehe ya kuchaguliwa | **19 April 2021** |
| Amechaguliwa na | **WAMILIKI WA KAMPUNI** |

**Sahihi** ........................................ **Tarehe: 22/10/2024**

**Jina: LINDA ALLAN MWAMBETE**

# Tembo wavamia makazi, waua watu watano

**Na Ashton Balaigwa,**

WATU watano wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa baada ya kushambuliwa na tembo waliovamia mashamba na makazi ya watu katika vijiji mbalimbali wilayani Liwale, mkoani Lindi katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu.

Imeelezwa kuwa wanyamapori hao, katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Oktoba mwaka huu, wamefanya uharibifu wa hekta 14,000 za mazao mbalimbali, yakiwamo ya chakula na biashara ya zaidi ya wananchi 4,000 katika wilaya hiyo ya Liwale.

Ofisa Maliasili na Mazingira Wilaya ya Liwale, Deogratias Simwanza, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliotembelea wilaya hiyo kuangalia utekelezaji Mradi wa Kupunguza Migongano ya Binadamu na Wanyamapori unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa niaba ya Serikali ya Ujerumani.

Simwanza alisema vifo hivyo vilitokea kutokana na kuwapo changamoto ya mgongano kati ya binadamu na wanyamapori na kusababisha wanyama hao wakali kuleta madhara na kugharimu maisha ya binadamu.

Alisema pamoja na kuwapo madhara hayo kwa binadamu, upo utaratibu wa kutoa fidia na kifuta machozi ingawa hauwezi kufananishwa na thamani ya binadamu. Wizara ya Maliasili na Utalii hutoa malipo baada ya tathmini inayofanywa na wilaya.

Alisema kuwapo migongano ya binadamu na wanyamapori wilayani Liwale kunachangiwa na eneo kubwa ya wilaya hiyo kuwa hifadhi na maeneo hayo yamehifadhiwa vizuri, hivyo kuwapo ongezeko la wanyamapori, hata wanafika katika makazi na mashamba ya wananchi.

"Tumekuwa na ongezeko kubwa la wanyamapori kwa sababu takribani vijiji vyote vimezungukwa na hifadhi, inachangia kuwapo migongano baina ya binadamu na wanyamapori na kutusababishia madhara, vikiwamo vifo," alisema Simwanza.

Mratibu wa Mradi wa Utatuzi wa Migongano ya Binadamu na Wanyamapori kutoka GIZ Wilaya ya Liwale, Debolah Missana, alisema mradi huo unakusudia kupunguza tatizo hilo na tayari umeanza kufanya kazi katika vijiji 11 na umepata mafanikio ya kuanza kudhibiti tembo kuingia katika mashamba ya wakulima pamoja na makazi ya watu.

Alisema moja ya hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto hiyo ni kuwapa mafunzo wahifadhi kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), hata kufundishwa kuendesha ndege nyuki kwa ajili ya kufukuza tembo kidigitali.

Alisema njia nyingine ambayo hivi sasa wanaanza kuitekeleza kufukuza tembo mashambani ni kutumia mizinga ya nyuki na tayari GIZ wameshatoa mizinga 100 kwa wilaya ya Liwale na wanatarajia kuongeza mingine 200.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Goodluck Mlinga, alithibitisha vifo hivyo, akisema tembo hao kusababisha madhara kunatokana na eneo kubwa la wilaya hiyo kuzungukwa na hifadhi, zikiwamo Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Pori la Akiba Selous, hifadhi za vijiji na jumuiya za hifadhi pamoja na maeneo ya uvunaji miti ya mbao.

Alisema kuwa kutokana na uhifadhi mzuri, wanyamapori wameongezeka kwa kasi, vijiji 64 vina changamoto kubwa ya kuvamiwa na makundi ya tembo (ndovu).



Dereva wa Bajaji akiwa ameisheheni mzigo kupita uwezo wake katika Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Mwisho, Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wahariri wampa waziri madai yao

**Na Jenifer Gilla**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF), limesikitishwa na kitendo cha Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, kutohudhuria matukio muhimu ya waandishi wa habari anayoalikwa.

Miongoni mwa matukio hayo ni Mkutano Mkuu wa Nane wa TEF uliofanyika jana, jijini Dar es Salaam na badala yake alimtuma mwakilishi kwa madai ya kutingwa na majukumu mengine.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano huo, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema wanasikitishwa na Waziri wa Habari kushindwa kuitikia mwito huo, akitaja mwaliko mwingine aliotoa udhuru kuwa ni Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT) za mwaka 2023.

Balile alimfananisha waziri huyo na mchungaji mwema ambaye anapaswa kuwafahamu kondoo wake ambao ni pamoja na tasnia ya habari, hivyo anapaswa kukaa nao mezani ili kufahamu tabia zao.

"Amealikwa Arusha, PRST (Jumuiya ya Maofisa Uhusiano) hakwenda, akaalikwa tuzo za waandishi habari hakwenda, nikasikia amealikwa Mbeya hakwenda, tukasema basi tumpe nafasi tumwalike akutane na sisi, hakuja, anasema Spika amenizuia," alisema.

Balile alionesha kushangazwa na waziri huyo kutohudhuria matukio hayo wakati Rais Samia Suluhu Hassan, alikutana na wahariri mara mbili, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mara tatu na wengine ni Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko na Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi.

Alisema hata Waziri wa Habari aliyepita Nape Nnauye, alikuwa mstari mbele, kila walipomhitaji alihudhuria bila kukosa haijalishi ni muda gani.

"Mwenendo huu tulisema hautufurahishi, hatutaki kugawana mbao katikati ya bahari, wala hatusemi kama hatujaribu, lakini akisema anataka huo mkondo sisi tupo tayari," alisema.

Hata hivyo, Balile alimshukuru waziri huyo kwa kuteua Bodi ya Ithibati ikiwa na wakongwe katika tasnia ya habari, ambayo itafanya utekelezaji wa Sheria ya Habari, jambo lililoshindikana tangu mwaka 2016.

Kuhusu malengo ya mkutano huo, alisema ni kutokana na maazimio yatakayoviwezesha vyombo vya habari kufanya kazi kwa weledi na kusimamia msingi mkuu ambao ni kutoa taarifa za kweli.

Alisema watajadili namna ya kuripoti Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kitaaluma zaidi ili kuhakikisha nchi inaingia katika uchaguzi na kumaliza ikiwa na umoja.

Balile alisema watajadili na kutoka na maazimio na namna ya kufanya ili kuviokoa vyombo vya habari na janga la kiuchumi wanalokabiliana nalo hivi sasa.

Alimshukuru Rais Samia kwa kupandisha uhuru wa vyombo vya habari kutoka nafasi ya 143 hadi ya 97 mwaka huu, kwa kutoa maelekezo mahususi ya kupunguza baadhi ya mambo yaliyokuwa yakiminya uhuru wa vyombo vya habari.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nicholaus Mkapa, alitoa wito kwa waandishi wa habari kuzingatia weledi na maadili ya kazi wanaporipoti matukio ya uchaguzi ili kuepuka kuandika habari za uzushi na kuhatarisha amani ya nchi.

Alisema historia inaonesha katika kipindi cha uchaguzi kunakuwa na habari nyingi za upotoshaji na changamoto kubwa zaidi zinatokana na kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Aliitaka TEF kuhakikisha inatoa maazimio ya kitaaluma yatakayoweka mkazo katika weledi, sheria na maadili ya uandishi wa habari wakati wa utekelezaji majukumu, ili kujenga uaminifu na uhalali mbele ya umma wanaoutumikia.

Pia, aliwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao kuwaonesha Watanzania maendeleo yanayofanywa katika nchi yao, ikiwamo mafanikio ya miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa treni ya kisasa na Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere.

Alisema serikali inaendelea kufanyia kazi madeni ya vyombo vya habari chini ya maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na kampuni ambazo hazijapeleka nyaraka za madeni yao, zifanye hivyo ili mchakato ukamilike kwa muda tarajiwa.

Alisema suala la umiliki wa hisa wa asilimia isiyozidi 49 kwa wageni katika kampuni za habari ni la kisera, hivyo linahitaji kufanyiwa marekebisho na mchakato wa kufanya marekebisho ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2013, umeanza na wataendelea kushirikishwa.

Alisema kuwa kwa kushirikiana na vyombo vya habari, wanaendelea kuboresha mifumo ya kisheria ikiwamo uanzishwaji Bodi ya Ithibati.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, aliwashauri waandishi wa habari wanapotekeleza majukumu yao, wadumishe amani kwa kutoa taarifa za kweli na kuzingatia haki na ukweli.

"Huwezi kuzungumzia amani kama huna upendo, ukiwa na chuki huwezi kumwelezea mtu yeyote kuhusu ukweli au amani. Matokeo ya amani ni maendeleo," alisema.

## Ubalozi Ufaransa wafungua kituo utoaji Visa ofisi za TLS

**Na Mary Geofrey**

UBALOZI wa Ufaransa nchini umefungua kituo cha kuomba Visa ya kusafiri kwenda Ufaransa katika ofisi za Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS).

Lengo la kuhamishia huduma za Visa katika kituo hicho ni kuzirahisisha na kupunguza msongamano katika ofisi za ubalozi huo.

Balozi wa Ufaransa nchini, Anne-Sophie Ave, akizungumza na waandishi wa habari wakati akizindua kituo hicho jijini Dar es Salaam, alisema kupitia kituo hicho waombaji Visa wanaweza kufanikiwa ndani ya wiki mbili.

"Tunayo furaha kuzindua kituo hiki katika ofisi za TLS, lengo ni kutoa huduma bora zaidi na kwa wakati mwafaka," alisema Balozi Ave.

Aliwataka waombaji kuanza kufuatilia huduma hiyo mwezi mmoja kabla, ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea mteja anapokuwa nje ya muda.

Balozi Ave alisema kuanza kutolewa huduma hizo katika kituo hicho kuna maana hazitapatikana katika ofisi za ubalozi huo.

"Wateja wetu wanapokuja kutafuta Visa watapata huduma kwa gharama zilezile," alisema. Aliwasihi wateja wao, wakiwamo watu mashuhuri, kutosita kufika kupata huduma hiyo kwa kuwa wana huduma ya VIP.

Meneja wa kituo cha hicho kipya cha kuombea Visa cha TLS Dar es Salaam, Abdillah Kinyaga, alisema mteja anayeomba Visa, anapaswa kuanza kuomba huduma hiyo mtandaoni na baadaye kufika katika ofisi hiyo kuendelea na hatua zinazofuata.

"Ni hatua kubwa kwa TLS kuingia makubaliano na Ubalozi wa Ufaransa kuanza kutoa huduma hii, tumechukua mzigo mkubwa ambao ulikuwa unafanywa na ubalozi katika ofisi zao," alisema Kinyaga.

Aliwahakikishia wateja wao kuwa, huduma hiyo inapatikana kwa haraka zaidi kwa kuwa wana watoa huduma wa kutosha waliobobea kutoa huduma hiyo.

Alisema wamebobea pia katika masuala ya kiusalama wa huduma wanazotoa na ndio sababu ya kuendelea kuaminiwa na ubalozi huo.

Akizungumzia aina ya Visa wanazotoa, alisema kuna aina mbili ambazo ni Schengen inayoruhusu mtu kusafiri zaidi ya nchi 29 na ya Ufaransa inatoa rukhsa mtu kwenda nchi hiyo moja pekee.

UCHAGUZI UJAO

# 'Wagombea wawekewe ulinzi wakati wa kampeni'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Mbongwe (CCM), Nicodemas Maganga, ameitaka serikali kuwalinda wagombea wakati wa kampeni za uchaguzi ili kumaliza salama mikutano katika maeneo yao.

Maganga akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, alisema mwaka huu ni wa uchaguzi na sheria zinaruhusu maandamano na mikutano, hivyo akahoji mpango wa serikali kuhakikisha inawalinda wanasiasa ili kumaliza mikutano salama.

Pia alisema kumekuwa na matukio ya wananchi kuchonganishwa na Jeshi la Polisi na wanaofanya matukio hayo ni watu wengine wakitumia mgongo wa jeshi hilo, hivyo kutaka kauli ya serikali kuhakikisha askari wanalindwa dhidi ya uchonganishi huo.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, akijibu maswali hayo, alisema Tanzania inaongozwa kwa mujibu sheria na utaratibu na kama kuna watu ambao ama wanafanya fujo au kuchonganisha Jeshi la Polisi, waache mara moja na watakaobainika, sheria itachukua mkondo wake ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Katika swali la msingi, Maganga alihoji mpango wa serikali kuhakikisha raia wa kigeni hawashiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Akijibu swali hilo, Sillo alieleza raia wa Tanzania ndiyo wenye haki ya kushiriki katika uchaguzi kwa kupiga kura au kuchaguliwa kuwa viongozi kwa mujibu wa sheria.

Alifafanua kuwa sheria hizo ni pamoja na ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 na ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 na kanuni zake za mwaka 2024.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa katika kusimamia vipindi vyote wakati wa uchaguzi, serikali imekuwa inatoa elimu ya uraia kwa watendaji (waandikishaji na wasimamizi wa uchaguzi) ili kuhakikisha raia wa Tanzania wenye sifa ndiyo wanaoshiriki uchaguzi na siyo raia wa kigeni.

"Inapobainika kwamba kuna mtu anadiriki kujiandikisha au kutafuta fursa ya kugombea na zipo taarifa au tuhuma, kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi, mhusika huyo huwekewa pingamizi," alisema.

Alisema kuwa ikithibitika, mtu huyo huchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kuondolewa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura na kufikishwa mahakamani.



Mwanafunzi wa fani ya umeme kutoka Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) mkoani Pwani, Peter Archard (kushoto), akitoa maelezo kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation, Asma Mwinyi (kulia), kuhusu mifumo mbalimbali ya nishati inavyofanya kazi, wakati wa mahafali ya 14 ya chuoni hapo jana. Wa pili kulia ni Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Clara Kibodya. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# TBS yajivunia ufanisi kuzuia vyakula visivyokidhi vigezo kuingizwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limezuia bidhaa nyingi za vyakula zisizokidhi vigezo vya usalama na ubora kuingia nchini, likiwataka wanaoingiza kuhakikisha bidhaa zina ubora.

Kwa uzuiaji bidhaa hizo, TBS imelinda na kuendeleza afya ya jamii na soko la Tanzania dhidi ya bidhaa za chakula zisizo na usalama na ubora. Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, David Ndibalema, wakati wa mkutano wa TBS na waingizaji vyakula nchini.

Ndibalema alisema tangu TBS ipewe jukumu la kusimamia sheria ya usalama wa chakula nchini, kwa kutumia dirisha la usajili katika kumlinda na kuendeleza afya ya mlaji, imepiga hatua mbalimbali ambazo zimeweza kuzuia bidhaa za chakula zisizo na usalama na ubora kuingia nchini wala kusambazwa sokoni.

Alisema usajili wa bidhaa za vyakula vilivyofungashwa ni takwa la kisheria linalolenga kuhakikisha vyakula salama na bora ndivyo vinaruhusiwa kuingizwa sokoni ili kulinda na kuendeleza afya ya mlaji na jamii kwa ujumla.

Alisema usajili huo pia unasaidia kulinda na kuendeleza biashara kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa na sera za nchi za kiuchumi zilizoko, hasa zile zinazohusu uwezeshaji wa kuwapo mazingira mazuri ya ufanyaji biashara.

"Nimefurahi sana kushiriki mkutano huu wa wafanyabiashara wanaoagiza na kuingiza bidhaa za chakula kilichofunganishwa nchini, mwitikio wenu ni ishara kuwa mkutano huo una umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kuwa bidhaa zinazotengenezwa na viwanda husika kisha kuingizwa nchini, usalama na ubora wake unafahamika kwa kutumia vigezo vya kisayansi bila kukwamisha ufanyaji biashara.

"Lengo kuu ni kulinda na kuendeleza afya ya mlaji pamoja na kulinda soko la Tanzania dhidi ya bidhaa za vyakula visivyo salama na bora," alisema Ndibalema.

Alisema mkutano huo utatoa fursa kupata uelewa wa pamoja ili shughuli za kusimamia usalama wa chakula nchini ziwe zenye ufanisi kupitia nguvu ya pamoja baina ya wafanyabiashara, walaji na wasimamizi.

Ndibalema alisema matarajio ya shirika hilo ni kwamba, mkutano huo utasaidia kuongeza ufahamu wa mambo mbalimbali kutoka kila upande, ikiwamo mwingizaji bidhaa kufahamu sababu za bidhaa yake anayotaka kuingiza nchini kukataliwa usajili na kujua tathmini zinazofanyika kwa bidhaa kukataliwa kusajiliwa.

Meneja wa Usajili wa Bidhaa na Majengo wa TBS, Habakuki Kalebo, alisema wamekuwa wanapokea maoni na maombi mbalimbali kutoka kwa wadau wa shirika yanayohusu namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika utendaji wao na kuboresha huduma zao kwa jamii wanayoihudumia.

Alisema moja ya mbinu ambayo itachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma kwa wateja na kwa wakati huo kuongeza ufanisi wa majukumu waliyopewa kisheria, ni kuwa na mikutano rasmi ya mara kwa mara na wadau wao, wakiwamo wafanyabiashara wanaoingiza nchini bidhaa zinazosajiliwa na TBS.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tanzania inahitaji masoko ya kimataifa

**MACHI** 21, 2018, nchi za Afrika zilisaini mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara (AfCFTA), ambalo linakadiriwa kuwa na watu zaidi ya bilioni 1.2 na pato la dola za Marekani trilioni 2.5 kwa mwaka.

Vipo vigezo ambavyo vitawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kulifikia soko hilo na masoko mengine ya kimataifa ambayo yanaruhusu nchi nyingine kuuza huduma na bidhaa zake nchini.

Moja ya kigezo ni kuwa na biashara iliyosajiliwa ambayo inatunza kumbukumbu zake za kifedha, mauzo, ununuzi, uzalishaji (kwa wenye viwanda), na namna wafanyabiashara wanavyozingatia ajenda ya dunia ya maendeleo endelevu kwa sekta zote.

Hapa nchini, zipo mamlaka na taasisi zinazoratibisha masuala ya biashara na kuthibitisha uhalali wake, ambazo ni muhimu wananchi wazitumie kikamilifu ili AfCFTA na masoko mengine yawanufaishe Watanzania.

Moja ya taasisi hiyo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ambayo inasajili kampuni, majina ya biashara, nembo za biashara, leseni za viwanda, miliki ubunifu na uvumbuzi (hataza).

Takwimu za BRELA zinaonyesha kwamba ni Watanzania wachache wanaomiliki biashara changa, ndogo na za kati wanaoona umuhimu wa kuzisajili. Kibaya zaidi ni kwamba ni wavumbuzi wachache zaidi, wanaojisajili kwa wakala huo.

Jambo la kusikitisha ni kwamba gharama za kujisajili zinahimilika ukilinganisha na hasara ambayo mtu anaweza kuipata kwa kutoilinda biashara yake kisheria.

Mathalani, kiwanda kidogo chenye mtaji wa chini ya Sh. milioni 10, kinachosindika unga, viungo au kinazalisha mafuta kinasajiliwa kwa Sh. 50,000 inayolipwa mara moja tu katika uhai wake wote.

Kwa wavumbuzi, ada ni Sh. 22,000 inayolipwa kwa awamu mbili na Sh. 4,000 kila mwaka baada ya kusajiliwa. Hiki ni kiasi kidogo ambacho bila shaka, Mtanzania mwenye nia ya kufanyabiashara kwa uaminifu, anamudu kuilipa.

Kama tunavyofahamu, mazingira ya Afrika kwa maana ya changamoto zinazoikabili jamii zinafanana kwa kiasi kikubwa; inasikitisha kuona mtu anabuni kitu kinachoweza kutatua changamoto kwenye jamii, anakiweka mtandaoni, anakipa na jina, bila kulinda jina wala uvumbuzi wenyewe.


Hali ni hiyo hiyo wakati wa maonyesho ya biashara kama ya Kimataifa ya Sabasaba ambayo yako mbioni kuanza; unakuta mbunifu anaeleza hatua kwa hatua namna alivyofanikiwa kubuni zana fulani ya kuwasaidia wakulima au wananchi katika sekta muhimu, baada ya maonyesho hanufaiki na ubunifu wake kwa kuwa wajanja wachache wanaamua kwenda kuisajili BRELA na kuanza kuizalisha. Hii ni hasara sio kwake pekee bali kwa nchi pia.

Mpango wa serikali wa kuboresha mazingira ya biashara nchini umeweka njia rahisi za kujisajili ambayo ni kupitia mtandao (ORS), unapata huduma zote za kurasimisha biashara yako ukiwa sehemu yoyote yenye intaneti.

Tunaeleza haya ili kuukumbusha umma kwamba wajasiriamali wetu wanaweza kuzalisha bidhaa nzuri, kutoa huduma bora, tukajitangaza mtandaoni lakini mwisho wa siku, tutakuta kile tunachouza kimelindwa kisheria na mtu mwingine; ambaye atakuruhusu kuendelea kutumia nembo au jina ulilobuni, kwa kumlipa mamilioni ya fedha kwa kuwa tu ameshajisajili.

Sheria itamlinda ambaye ameitii. Hata kama utakuwa mwanzilishi wa huduma, jina, uvumbuzi au nembo, usipoisajili halafu akatokea mgeni akaisajili nchini, hutaweza kujitetea kwa sababu hutambuliki kwenye mifumo ya kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tatizo la watoto mitaani liko kijamii mno, mhusika mzazi

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWAPO** na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani wanaolala nje ya maduka usiku nchini hasa kwenye majiji mkubwa.

Hilo limemshtua Mbunge wa Kilombero, Abubakar Assenga, akalizungumza bayana bungeni wakati akichangia Maendeleo ya Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26.

"Watoto wanakwenda mitaani na yatima wamezidi, hivi sasa tuna utamaduni wa kujenga vituo vya kulelea yatima na hatulei watoto yatima kwenye nyumba zetu. Hatuwezi kufikia maendeleo ya kweli, kama tunaongeza watu kiholela kwa namna hiyo," alisema.

Hilo la mbunge huyu, limenisukuma kuongea vitu ambavyo siku zote nilikuwa najiuliza kama yeye.

Serikali kwa kiasi chake imekuwa ikijitahidi sana kudhibiti watoto wa mitaani, kwa kuwachukua na kwenda kuwalea kwenye vituo vyao.

Taasisi za kidini, pia zimekuwa mstari wa mbele kuisaidia serikali, kwani zimekuwa zikiwatwaa watoto hao kuwapeleka kwenye vituo vilivyopo kwa ajili ya kuwahudumia ya msingi.

Wanawapa elimu, wanawajenga kisaikolojia, burudani wanapata na stadi za kazi, ili kuwafanya wajione wapo kama binadamu wengine wa kawaida.

Kumbuka watoto hawa wa mitaani au yatima wanakuwa wameathirika kisaikolojia, pale wanapoona wenzao wana wazazi lakini wao hawana, wametelekezwa, au kukimbia makwao kutokana na sababu mbalimbali.

Lawama kubwa hapa ziende kwenye familia. Matatizo makubwa ya yote haya yanasababishwa na familia, ambazo ndizo zimewapata hawa watoto katika mazingira ambayo hajaandaliwa na kuleta tabu. Kingine ni kwamba, jamii zetu za sasa, kuanzia familia, ndugu na marafiki kuwa wabinafsi.

Miaka ya sasa watu wengi wamekuwa wabinafsi sana tofauti na wa zamani.

Hayo yote ndiyo wamesababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Ngono zembe zinasababisha kupatikana kwa watoto wasiotarajiwa, ambao wazazi wa pande zote mbili baba na mama kwa sababu hawajajiandaa, wanashindwa kuwapa malezi mema.

Mwanaume anaweza kuikataa mimba, au kumtoroka mwanamke ambaye naye hata kama akikifungua anashindwa kulea mtoto wake na mara nyingi mtoto wa kike anakuwa ametengwa na familia.

Mateso ya walezi hasa ambao wameachiwa jukumu la kulea baada ya wazazi kufariki, yanasababisha watoto kukimbia na kuingia mtaani ambako wanaona wapo salama.

Wengine wanakuwa wamefukuzwa na walezi wao, hasa ndugu za baba na mama zao baada ya wazazi yao kufariki.

Zamani ndugu akifariki, jukumu la malezi linakuwa kwa ndugu ambao walikuwa wakipeana majukumu ya kuwalea watoto kwa mpangilio ambao wao waliona unafaa.

Acha ndugu, hata marafiki na majirani kipindi cha nyuma walikuwa wanaweza kuwatunza na kuwalea watoto ambao wazazi wake wamefariki, kiasi kwamba hawataki mwingine kujua kama hawana wazazi.

Ubinafsi wa kizazi cha sasa kukumbatia familia zao pekee, pamoja na dai la ugumu wa maisha, umewafanya wengi kushindwa kuwasaidia watoto wa mitaani, yatima wanaolala nje ya maduka na chini ya madaraja.

Ni wakati sasa wa kila mmoja kuchukua nafasi yake kifalsafa na kimatendo. Serikali na taasisi ya dini ziendelee kulea watoto, lakini huku kwenye ngazi ya familia, watu waache ngono zembe, ili kuepuka kuongezeka kwa watoto wa namna hiyo. Pia, jamii zisikwepe majukumu yao, kwani kulea watoto hao wa ndugu, jamaa na marafiki ni wajibu wao wa msingi.

HABARI KITAIFA

# Tanzania yaalika wawekezaji sekta ya nishati

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Nishati imetumia jukwaa la Mkutano wa Wiki ya Nishati Afrika unaofanyika Cape Town, Afrika Kusini kueleza fursa za uwekezaji zilizoko katika sekta ya nishati.

Pia imetumia jukwaa hilo kukaribisha wawekezaji kuchangamkia fursa zilizoko katika sekta hiyo Tanzania.

Katika wasilisho lake juzi, Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia mafuta na gesi, Dk. James Mataragio, alibainisha fursa katika maeneo mbalimbali ikiwamo uwekezaji katika vitalu vya utafutaji mafuta na gesi asilia, miundombinu ya mafuta na gesi, miradi ya nishati jadidifu na viwanda vya petrokemikali.

Katika eneo la vitalu vya utafutaji mafuta na gesi asilia, Dk. Mataragio alieleza kuwa tayari wizara imekamilisha maandalizi muhimu kuelekea uzinduzi wa duru ya tano ya kunadi vitalu hivyo vya mafuta na gesi asilia vilivyo wazi Machi mwakani.

"Tunatarajia kunadi jumla ya vitalu 26 vya utafutaji mafuta na gesi asilia nchini. Kati ya vitalu hivyo, vitalu 23 vipo eneo la baharini na vitatu vipo eneo la Ziwa Tanganyika," alisema Dk. Mataragio.

Alisema ipo fursa kwa wawekezaji kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuendeleza vitalu vya Eyasi-Wembere, Mnazi Bay Kaskazini na Songo Songo Magharibi, vitalu ambavyo shirika hilo limeendelea kuvifanyia utafiti wa mafuta na gesi asilia.

Katika wasilisho hilo, Dk. Mataragio alisema data za vitalu vyote vitakavyopelekwa katika mnada na vile vinavyoendeshwa na TPDC, zinapatikana kwa ajili ya wawekezaji kuona na kununua na kwamba miongoni mwa aina za data hizo ni pamoja na nguvu sumaku ya miamba, uzito wa miamba, mitetemo na visima.

Maeneo mengine ya uwekezaji aliyoyataja katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia ni uwekezaji katika ujenzi wa vituo vya kujaza gesi asilia katika magari na viwanda vya petrokemikali kwa kutumia gesi asilia.

Dk. Mataragio alieleza kuwa serikali imefanya kazi kubwa kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini na kutekeleza miradi ya kimkakati ukiwamo ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) na kwamba Tanzania ni sehemu sahihi kwa uwekezaji.



Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Elisha Mnyawi, akizungumza kuhusu mikakati ya uongozi wake katika kuwajengea uwezo wachimbaji, wakati wa kikao cha wadau wa madini ya Tanzanite, katika mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kilichojificha Dodoma kuipiku Dar matumizi dawa za kulevya

**Na Maulid Mmbaga**

WASAIKOLOJIA tiba na wataalamu wa afya ya akili wameeleza kwamba kukua kwa mji, kuongezeka idadi ya watu pamoja na shughuli za kiuchumi, ni miongoni mwa sababu kuu zinazosababisha mkoa wa Dodoma kuwa na kiwango kikubwa cha matumizi ya dawa za kulevya.

Hivi karibuni, Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Peter Patric, alibainisha kuwa mkoa wa Dodoma unakuja juu kwa kiwango kikubwa cha matumizi ya dawa za kulevya, ikiwamo aina ya Heroine, ikipiku Dar es Salaam iliyokuwa inaongoza awali.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mtaalamu wa Masuala ya Afya ya Akili kutoka Taasisi ya Bodymind Insights, John Amros, alisema mbali na kuongezeka kwa biashara za kiuchumi katika mkoa huo, mkoa huo hivi sasa unapokea idadi kubwa ya vijana wanaoingia katika harakati za utafutaji kutokana na ukuaji wa kiuchumi na rasilimali.

"Katika hatua hizo, kuna matarajio mengi, mji unajengwa tunategemea vijana ambao wanaingia katika sekta ya ujenzi ni wengi, na kuna uhusiano wa karibu sana na matumizi ya dawa za kulevya hususani bangi, hasa kwa wanaofanya kazi ngumu, wakiwamo vibarua wa ujenzi.

"Ukiangalia idadi ya mafundi na vibarua wanaofanya kazi za ujenzi wa nyumba na miundombinu mingine Dodoma, ni kubwa.

"Hivyo haitakuja kuonekana kuwa ni suala tu la dawa za kulevya pekee, bali pia utafiti mwingine unasapoti kwamba maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) nayo yatapanda," alisema Amros.

Mtaalamu hiyo ambaye ni msaikolojia tiba, aliongeza "Mimi pia ninaunga mkono kwamba katika mkoa huo ongezeko litazidi kuwa kubwa kutokana na hatua mbalimbali za ukuaji wa eneo lile, sisemi kwamba wanaojenga wote wanatumia lakini kwa uzoefu wangu niliwahi kuajiri watu, walivyomaliza ujenzi, baada ya muda pale mahali paliota bangi," anasema.

Alieleza kuwa kuna utaratibu kwa baadhi ya vijana kufanya kazi, akishalipwa huenda kutumia vileo, fedha ikiisha ndipo wanaonekana tena, akihadharisha kwamba hiyo ni changamoto na ni tatizo la kisaikolojia ambalo linahitaji elimu itolewe kwa umma hasa kwa rika hilo.

Pia alishauri kwamba makandarasi wanapopewa miradi, pawapo kipengele cha kutoa elimu ya VVU/Ukimwi na dawa za kulevya, sambamba na kuwekwa makubaliano kati ya mamlaka za udhibiti na taasisi zinazoajiri watu hao ili kuhakikisha wanakuwa na sera au miongozo ya kuelimisha umuhimu wa kuelewa madhara ya dawa hizo.

"Tunapoteza nguvu kazi ya taifa kwa sababu ya watu kujiingiza katika matunizi ya dawa za kulevya. Ukangalia sasa hivi changamoto ya afya ya akili ni kubwa, vijana wameingia katika matumizi ya dawa na vilevi vikali vya bei rahisi," alionya Amros.

Mtaalamu mwingine wa Saikolojia na Afya ya Akili kutoka Somedics Polyclinic, Saladin Kimangale, alisema ongezeko hilo ni athari za maendeleo ya mkoa huo, akieleza kwamba katika eneo lolote linalokuwa na mwingiliano wa watu, wanakuja na tabia tofauti kutoka maeneo mbalimbali wanakotoka.

Alisema hali hiyo pia inaweza kuchangiwa na tabia ya watu kutumia dawa za kulevya kama sehemu ya starehe, huku wengine wakizitumia kama njia ya kujituliza dhidi ya maumivu fulani.

"Vijana wengi hawana maarifa ya kutatua changamoto zinazowakabili, hawawajibiki, hali hiyo inawafanya kujiingiza katika vitu kama hivyo.

"Ninashauri wajiepusha na kuiga utamaduni au vitu wanavyoviona maeneo mengine, pia mamlaka ziongeze nguvu katika udhibiti pamoja na vijana kuongezwa shughuli za kufanya zitakazowasaidia kuwa 'bize'.

"Kumwondoa mtu katika matumizi ya dawa za kulevya ni jambo gumu, hivyo ni lazima elimu ianze kutolewa kuanzia ngazi za chini," alisema Amros.

Alisisitiza elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya lisiwe jukumu la Kamishma wa DCEA pekee, bali uwe wajibu wa woten na kuwe na miongozo ya kuwawajibisha wale waajiri ambao maeneo yao ya kazi yataonekana kuwa na viashiria vya kuwapo dawa za kulevya.

Pia alishauri elimu ipelekwa shuleni ili watoto wajifunze madhara ya afya ya akili na dawa za kulevya, na suala hilo liwe shirikishi, kamisheni zishirikiane zisiwe ni kwa ajili ya tume na kuwe na utaratibu wa elimu kwa umma ambao utawezesha vijana kuwa na uelewa na kuachana na dawa hizo.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# 'Waliozamia Sauzi' wahukumiwa kulipa faini 40,000/-

**Na Grace Gurisha**

VIJANA 64 wamehukumiwa kulipa faini ya Sh. 40,000 kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya kuondoka nchini kwenda Afrika Kusini kinyume cha sheria na wakishindwa kulipa, watatumikia kifungo cha miezi sita gerezani.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni pamoja na Abdallah Ramadhani (29), Abdul Rajabu (49), Abdul Lusambi (23), Abdulrahman Mtimbe (38), Abubakar Feruz (28), Abubakar Kitemba(29), Abuu Kabaga (28) na Adam Kiselekela (31).

Wengine ni Adam Mkumba (30), Akida Ally (24), Ally Maduka (24), Ally Ally (42), Ally Mpene (28), Ally Mohamed (36), Amary Hemed (27), Ashrafu Matata (30), Athuman Ramadhan (18) na wengine 47.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam baada ya washtakiwa wote kukiri mashtaka dhidi yao.

**Alidai kuwa Oktoba 29, 2024, washtakiwa, wakiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, wakiwa wamerejeshwa kutoka Afrika Kusini walikokwenda kwa tarehe tofauti bila kufuata**

Alisema kutokana na washtakiwa kuwa wakosaji kwa mara ya kwanza na wanaonesha kujutia makosa yao, hivyo mahakama hiyo inawahukumu kulipa faini ya Sh. 40,000 kwa kila mmoja na wakishindwa kila mmoja atatumikia kifungo cha miezi sita gerezani.

Kabla ya adhabu hiyo kutolewa, washtakiwa waliomba mahakama iwapunguzie adhabu na isiwape adhabu kali na kuahidi hawatorudia kufanya makosa hayo.

Awali, akiwasomea washtakiwa mashtaka yao, Wakili wa Serikali Ezekiel Kibona, akisaidizana na Grace Nyarata, alidai wote wanakabiliwa na kosa moja.

Alidai kuwa Oktoba 29, 2024, washtakiwa, wakiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, wakiwa wamerejeshwa kutoka Afrika Kusini walikokwenda kwa tarehe tofauti bila kufuata taratibu na sheria za uhamiaji za kuondoka nchini.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, washtakiwa wote walikiri kutenda kosa hilo.

Baada ya kukiri, Wakili Kibona aliwasomea washtakiwa maelezo ya awali na kudai wote ni raia wa Tanzania ambao katika tarehe tofauti kupitia mipaka tofauti waliondoka nchini bila kibali.

Aliendelea kudai kuwa katika tarehe na majira tofauti, washtakiwa walikamatwa Afrika Kusini kwa makosa mbalimbali, ikiwamo kuishi katika nchi hiyo kinyume cha sheria.

Alidai kuwa Oktoba 29, 2024 washtakiwa wote waliondolewa Afrika Kusini na kurudishwa Tanzania na katika tarehe hiyo baada ya kufika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, walikamatwa na kushtakiwa kwa kosa la kuondoka nchini kinyume cha sheria.

Pia katika tarehe hiyo, washtakiwa wote walifikishwa katika ofisi za uhamiaji na baadaye kuambiwa haki zao za msingi na kuanza kuhojiwa na wote walikiri kutenda kosa hilo.

Novemba 4, 2024, washtakiwa wote walifikishwa mahakamani huko na kusomewa makosa yao yanayowakabili ambalo ni kuondoka nchini bila kufuata sheria za uhamiaji za nchi zinavyoelekeza.

Baada ya maelezo hayo, washtakiwa wote walikiri kuwa hoja hizo ni za kweli. Kibona aliomba mahakama iwape washtakiwa adhabu kulingana na makosa wanayoshtakiwa nayo.




Mkurugenzi wa Ibra Construction, Maida Waziri (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), waliofanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho katika hafla iliyofanyika chuoni hapo, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA:**

# Wadau wakutana kusuka Mpango wa Uhimilivu na Uendelevu wa UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

SERIKALI kwa ushirikiano na wadau wa maendeleo na watekelezaji shughuli za mwitikio dhidi ya UKIMWI, wamekutana mkoani Arusha kwa siku mbili kuandaa Mpango wa Uhimilivu na Uendelevu wa UKIMWI nchini.

Ni kikao kinachoratibiwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), mpango huo ukilenga kuweka mikakati itakayowezesha nchi kutekeleza afua za UKIMWI kwa fedha za ndani pale ambapo fedha kutoka kwa wafadhili zitapungua zaidi au kukoma kabisa. Mikakati inayowekwa ni ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu baada ya mwaka 2030 ambapo inatazamiwa kuwa UKIMWI utakuwa si janga la kiafya duniani.

Akizungumza katika kikao hicho, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, alisema kupatikana kwa mpango huo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuwa na uwezo wa kutekeleza afua za UKIMWI nchini, ikiwamo kuziba mwanya wa upungufu wa rasilimali za mwitikio wa UKIMWI nchini baada ya kuendelea kupungua kwa rasilimali za kutekeleza afua hizo.

"Mpango wa uendelevu wa mwitikio wa UKIMWI ni sehemu ya maandalizi ya kukabiliana na upungufu wa rasilimali za kutekeleza afua za mwitikio wa UKIMWI nchini.

"Ninawashukuru sana wadau wote mlioshiriki na kufanikisha maandalizi ya mpango huu, ni matumaini yangu kuwa sote tutashiriki siku ya uzinduzi utakaofika mkoani Ruvuma tarehe Mosi Desemba 2024 ili tushuhudie kazi tuliyoifanya kwa kipindi chote hiki inazinduliwa tayari kwa matumizi," alisema Dk. Kamwela.

Aliongeza kuwa kazi ya mapambano dhidi ya VVU bado kubwa kwa kuwa pamoja na kiwango cha kitaifa cha ushamiri wa maambukizi kupungua, ushamiri katika baadhi ya makundi umeongezeka, hasa miongoni mwa makundi ya wachimbaji wadogo wa madini, wavuvi, madereva wa masafa marefu pamoja baadhi ya mikoa nchini.

Hivyo, Dk. Kamwela akasema ni lazima waongeze juhudi hadi hapo watakapoona wanaondoa kabisa maambukizi mapya, watu wote walioambukizwa wanajitambua na kutumia dawa na kuhakikisha kunakuwa hakuna ubaguzi na unyanyapaa kwa WAVIU na wote walioathirika na UKIMWI. Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia UKIMWI (UNAIDS), Dk. Martin Odiiti, akizungumza katika kikao hicho, alipongeza jitihada za serikali kuona umuhimu wa kutoa kipaumbele katika maandalizi ya Mpango wa Uendelevu wa Mwitikio wa UKIMWI nchini.

Dk. Martin alisema kuwa hii ni nyenzo muhimu kwa nchi kwa kuwa huo ni mwanzo mzuri wa kuwezesha nchi kutekeleza mwitikio wa UKIMWI kwa fedha zake za ndani.

Hata hivyo, aliwahakikishia wajumbe wa kikao kuwa kuandaliwa kwa mpango huo hakumaanishi kuwa wafadhili na wadau wa maendeleo wataondoka nchini.

Kikao hicho kilihudhuriwa na wadau kutoka wizara, wadau wa maendeleo na watekelezaji Afua za Mwitikio wa UKIMWI.

## Serikali yajipanga kurejesha minada ya madini ya vito

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inatarajia kurejesha minada ya ndani ya madini ya vito katika maeneo ya uzalishaji ndani na nje ya nchi ili kuongeza pato la taifa kutokana na ukusanyaji kodi.

Mpango huo ulitangazwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Ramadhani Lwamo, wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Lwamo aliyataja maeneo ambako minada hiyo itafunguliwa kuwa ni pamoja na Mirerani, mkoani Manyara, Mahenge (Morogoro), Tunduru (Ruvuma), Dar es Salaam, Arusha na Tanga.

Kwa upande wa kimataifa, alisema serikali imepanga kufungua minada hiyo katika miji ya Bangkok na Jaipur huko India, akisisitiza kuwa uendeshaji minada hiyo ni fursa muhimu kwa serikali kutangaza vito na madini yanayozalishwa na kupatikana nchini.

"Uendeshaji minada hii ni fursa muhimu ya kutangaza madini ya vito vinavyozalishwa nchini hususan kwenye masoko ya kimataifa," alisema Lwamo na kuitaja ni hatua mojawapo ya kuwafikisha wananchi hususani wachimbaji wa madini hayo katika masoko ya uhakika na upatikanaji bei nzuri na stahiki.

Awali Kaimu Katibu Mkuu huyo alisema kuanzishwa masoko ya madini nchini kumedhibiti utoroshaji rasilimali hiyo na kuongeza uwazi katika sekta ya madini.

Alisema kuwa hadi sasa kuna masoko 44 na vituo 106 vidogo vya ununuzi wa madini vilivyoanzishwa nchini.

"Masoko haya yamesaidia kuweka mifumo ya kufuatilia na kusimamia biashara ya madini, ikiwamo teknolojia za kidijitali kusaidia kurekodi taarifa za madini kutoka kwa wachimbaji hadi kwa wanunuzi," alisema Lwamo.

Aliongeza kuwa kuanzishwa kwa masoko hayo, kumesaidia kudhibiti bei kwa kutoa bei elekezi, shindani na za haki, kulinganishwa na soko la dunia.

Alisema hatua hiyo pia imepunguza hamasa ya watu kutorosha madini kwa nia ya kuuza kwa bei kubwa zaidi kwenye soko la magendo.

"Masoko haya yamesaidia kuongeza mapato ya serikali kupitia tozo na ada zinazotozwa kwenye masoko haya," alisisitiza.



# Simanzi moto ukiua mtoto, kuteketeza nyumba

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

MTOTO wa mwaka mmoja na nusu, amekufa baada ya nyumba alimokuwa amelala kuteketea kwa moto uliosababishwa na mlipuko wa gesi wakati kaka yake mwenye tatizo la afya ya akili akiwasha jiko.

Baadhi ya mashuhuda akiwamo, Ismail Hosea, alisema tukio hilo lilitokea Novemba 5, mwaka huu katika Mtaa wa Madukani, Kata ya Sokoin 1 jijini hapa.

Hosea, alisema wao waliona moshi mzito umetanda juu ya nyumba hiyo yenye vyumba 10, na majirani wenzake walipofika walikuta ukiwaka kwenye moja ya chumba na kufanya jitihada za kuzima huku wengine wakiokoa vitu vilivyokuwa ndani.

"Hakuna aliyekuwa na wazo kama mtoto yumo ndani amelala sababu watoto wawili walikuwa wameokolewa japo kuna wanawake walikuwa wakipiga yowe kuashiria kuwa bado kuna mtoto," alisema.

Alisema mama wa watoto hao, anayetambulika kwa jina la mama God, amekuwa akiwaacha pekee yao nyumbani na kwenda kufanyabiashara ya mboga na viungo katika Soko la Kilombero jijini hapa.

"Walipofika watu wa zima moto na walitusaidia kuuzima moto huo kabla haujaleta madhara nyumba za jirani, tukaingia kupekua ndani kwenye masalia ya vitu vilivyoungua tukaona mtoto mdogo ameungua amebaki masalia, imeniuma sana," alisema na kuongeza kuwa: "Vitu vinatafutwa lakini uhai wa mtu haupatikani ukishapotea umepotea, wangekuwa na hakika ni bora wangeelekeza nguvu kumwokoa mtoto."

Zakayo Mollel, aliwashukuru wanawake kwa kupambana kuzima moto kabla ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kufika kuongeza nguvu na kufanikisha kuudhibiti kabla ya kusambaa kwenye vyumba na nyumba zingine.

Alisema mwili wa mtoto huyo umeteketea na kubaki fuvu la kichwa na tumbo na kuacha simanzi kwa watu waliojitokeza kuzima moto huo.

Irene John, alisema akiwa jirani aliona moshi mzito umetanda katika eneo hilo na baada ya kufika aliambiwa mtoto wa nyumba hiyo mwenye changamoto ya akili ni chanzo cha tukio hilo kwa kuchoma godoro na kukimbilia nje huku akimuacha mdogo wake ndani amelala.

"Kilichonisikitisha walipofika watu wa serikali sijui polisi, walibeba mabaki ya mtoto kwenye ndoo, hili sio jambo la kibinadamu huyu ni binadamu hakupaswa kubebwa kama nyanya," alisema.

Kaimu Kamanda wa Kikosi hicho Mkoa wa Arusha, Oswad Mwanjejele, alithibitisha nyumba hiyo kuungua moto.

"Tulifanikiwa kuuzima moto huo kabla ya kusambaa kwenye nyumba zingine za jirani na hapo nyingi," alisema Mwanjejele. Alisema katika uchunguzi wao wa awali, wamebaini chanzo cha moto huo ni jiko la gesi la mtungi wa kilo 15 kulipuliwa na mtoto anayedaiwa kuwa na matatizo ya afya ya akili.

Alisema inadaiwa mtoto huyo alikuwa anachezea mtungi huo na baadhi ya majirani walisikia harufu ya gesi kabla ya moto kuwaka na kusababisha madhara hayo.



Mkuu wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Elijerry, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Juma Mahunja (katikati), akiinadi keki katika mahafali ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kwemkabara, kwa ajili ya kukusanya fedha za kununulia mashine ya kudurufu ya shule hiyo. Wengine ni Diwani wa Kata ya Kwamkabara, Peter Mgavilwa (wa pili kulia), Mkuu wa Shule hiyo, Juma Hango (wa tatu kulia) na (wa nne kulia) ni Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, John Mdoe. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wachina wamiminika Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

IDADI ya watalii kutoka China wanaokuja nchini kutembelea vivutio vya utalii vikiwemo vya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imeongezeka kutoka 32,000 hadi kufikia 54,000 kwa mwezi Septemba mwaka huu.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema ongezeko hilo ni la kati ya mwaka 2018 kabla ya Uviko-19, Wachina walikuja nchini takribani 32,000 na baada ya uzinduzi wa filamu ya Amaizing Tanzania Mei mwaka huu, idadi hiyo imeendelea kuongezeka.

Waziri huyo, alisema filamu hiyo iliyoongeza chachu ya utalii ni jukwaa muhimu kutangaza urithi wa kipekee na vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania.

"Hii filamu imefungua milango zaidi kwa watalii na wawekezaji kutoka China, Bara la Asia na ulimwenguni kwa ujumla kuja Tanzania kuona vivutio vya utalii,"alisema.

Dk. Chana, alisema hadi mwakani, serikal i inatarajia kuona sekta ya utalii nchini, mapato yake yanaongeza hadi dola za Marekani bilioni sita na kufikisha idadi ya watalii milioni tano.

"Malengo ya Wizara yetu, kufika mwaka 2025 tunataka tuwe tumeongeza ukusanyaji wa mapato kufikia zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni sita na watalii zaidi ya milioni tano,"alisema.

Alisema katika mpango wa kufikia malengo hayo, kwa mwaka jana wamekusanya mapato zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni tatu, kasi hiyo inahakisi kufikia malengo yao.

"Tunaamini tutafikia lengo na kuvuka mpaka kufikia mwakani kwa kuwa mipango iliyopo ni kuhakikisha tunafungua kanda ambazo zilikuwa chini kiutalii ikiwamo ya kusini.

"Tutahakikisha tunaboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, barabara na kutangaza vivutio vilivyopo, itachangia kufikia lengo."alisema.

Alisema masoko ya utalii kutoka nchi za Brazil, China na India yamefunguka mbali na ya kimkakati ya Ulaya na Marekani.

# Serikali yatenga mabilioni uchanjaji wa mifugo

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 28 kuendesha kampeni maalum ya kitaifa ya kuchanja mifugo ili kufikia malengo ya mpango wa afya moja.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema katika kuimarisha mpango huo, serikali imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau kutekeleza hasa maeneo ya kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na milipuko ya magonjwa na hatari nyingine za afya.

Ulega, alidokeza kuhusu ujio wa kampeni hiyo akiwa jijini Arusha kwenye mkutano wa kitaifa wa afya moja.

Alisema kwa mara ya kwanza, serikali itaongoza uchanjaji mifugo nchi nzima, kama inavyofanya kwa afya ya wanadamu.

Lengo la dhana ya afya moja, ni kupanua na kuimarisha ushirikiano baina ya sekta na taaluma kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na milipuko ya magonjwa na hatari nyingine za afya katika kutekeleaji wa afua hizo.

"Ni wakati sahihi kuendelea kushirikiana na wadau wengine ikiwemo jamii kuhakikisha nguvu ya pamoja inatuvusha tulipo na kuendelea kuipa nguvu dhana ya afya moja," alisema

Afya moja ni dhana ya kimataifa iliyoridhiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya ya Wanyama (OIE), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Programu ya Kimataifa ya Mazingira (UNEP) kupitia Global Health Security Agenda (GHSA) na wadau wengine wa afya duniani.

WHO, OIE na FAO, yametoa wito kwa wataalamu wa sekta za wanyama na mazingira kuongeza na kuimarisha ushirikiano ili kuboresha ufanisi kukabiliana na tishio la magonjwa ya kuambukiza yanayoenea kutoka kwa wanyama.

# Balozi ahamasisha wananchi kupikia gesi

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI wilayani hapa Mkoa wa Tanga wamehamasishwa kutumia nishati safi kupikia majumbani ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu katika kampeni yake ya kutunza na kuhifadhi mazingira nchini.

Wito huo ulitolewa na Balozi wa Mazingira na Maendeleo nchini, Michael Msechu wakati wa ziara yake wilayani hapa na timu yake kuzunguka nchini kuhamasisha wananchi kupikia gesi na kutunza mazingira.


Msechu, alisema wako wilayani hapa kuhamasisha utunzaji wa mazingira na wananchi kujitokeza kuchagua viongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika nchini Novemba 27, mwaka huu.

Alisema wanaungana na vijana kutembelea miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia.

Kwa mujibu wa Msechu, Tanga umepata Sh. tirioni 2.8 kutekeleza miradi ya maendeleo ya maji, barabara shule, afya na umeme na mingine kwa manufaa ya wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, alisema kwa niaba ya viongozi wa wilaya, amemkabidhi cheti cha pongezi balozi huyo kwa kazi anayoifanya kwenda wilaya zote nchini kuzungumzia ajenda za maendeleo ya taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Jumaa Mhina, alisema kazi anayoifanya balozi huyo ni nzuri na wanamkaribisha tena wilayani hapa kuhamasisha jamii kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kujiongezea kipato.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Mtanda abeza wanaokimbia na masanduku ya kura

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amesema mambo ya kukimbia na masanduku yenye kura yamepitwa na wakati na kuwahakikishia wananchi, wadau mkoani hapo kuwa wamejipanga kuhakikisha uchaguzi wa serikali za mitaa utakuwa huru na wa haki.

Mtanda aliyasema hayo juzi wakati wa kongamano la viongozi wa dini mkoani hapa la kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kujitokeza kupiga kura katika uchaguzi huo utakaofanyika nchini Novemba 27, mwaka huu.

Katika kongamano hilo lililoshirikisha kamati ya amani ya viongozi wa dini mkoani hapa, Mtanda alisisitiza kuwa uchaguzi huo utafuata mchakato na hawana mpango wa kumzuia mgombea yeyote kuchukua fomu.

**"Kuhusu suala la amani, tumejiandaa kikamilifu kuhakikisha uchaguzi unapita salama na hakuna atakayeguswa kwa namna yeyote, wajibu wetu ni kukumbushana na kuhimizana suala la amani ili wachache wenye nia...**

Alisema kila mwananchi aliyejiandikisha katika daftari la mkazi, atapata fursa ya kupiga kura na kuhesabiwa kwa uwazi na kushuhudiwa na wakala wa kila mgombea na matokeo halali kutangazwa.

"Kuhusu suala la amani, tumejiandaa kikamilifu kuhakikisha uchaguzi unapita salama na hakuna atakayeguswa kwa namna yeyote, wajibu wetu ni kukumbushana na kuhimizana suala la amani ili wachache wenye nia ovu waache," alisema Mtanda.

Kwa upande wao viongozi wa dini mkoani hapa walikubali kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wanaowataka kama walivyofanya wakati wa kujiandikisha kupiga kura.

Mwenyekiti mwenza wa kamati hiyo, Sheikh Hassan Kabeke, aliwataka wananchi bila kujali dini zao kudumisha amani wakati wa mchakato wa uchaguzi huo wa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji nchini.

"Zipo taarifa wanawake hawakujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi, sasa twendeni tukawahamasishe wajitokeze kuchagua viongozi wanaowataka hususani wanawake ili kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye ngazi ya maamuzi," alisema Sheikh Kabeke.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Askofu Charles Sekelwa, aliwataka wananchi kuepuka kuchagua viongozi wala rushwa, la sivyo taifa litakosa maendeleo.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) cha Butiama, mkoani Mara, Prof. Lesakit Mellau (kushoto), akibadilishana nyaraka na Mwakilishi wa Kampuni ya M/S Shandong Hi-Speed Dejian Group Ltd ya China, Li Manchao baada ya kutiliana saini mkataba wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya chuo hicho, mjini Butiama juzi. Katikati ni Mkuu wa mkoa huo, Kanali Evans Mtambi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajerumani waipa ahueni SHUWASHA

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), inatarajia kutumia Sh.bilioni 9 kwa ajili ya kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi.

Mpango huo ulitangazwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Yusup Katopola, baada ya mamlaka hiyo kusaini mkataba), imesaini mkataba wa kiasi hicho cha fedha na Kampuni ya GOPAInfra ya nchini Ujerumani kwa ajili ya kutekeleza mradi huo na kuboresha utendaji kazi wao.

Katopola, alisema hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa majisafi na usafi wa mazingira Shinyanga kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania wenye thamani ya Euro Milioni 76.

Alisema katika mkataba huo, watafanya kazi kwa ushirikiano na kuhakikisha malengo ya Serikali ya uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira maeneo yanayohudumiwa na SHUWASA.

"Mkataba huu utatekelezwa ndani ya miaka minne kuanzia Novemba 4, 2024 hadi Novemba 2028 na utakuwa msaada mkubwa kwetu kutoa huduma bora kwa wananchi," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa GOPAInfra, Stefan Doerner, alisema lengo la mkataba huo ni kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi wa Shinyanga na kuboresha utendaji wa mamlaka hiyo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Superlit Consulting LTD Tanzania, Mhandisi Fortunatus Kasimbi, ambao watafanya kazi na GOPAInfra kuijengea uwezo SHUWASA, alisema mkataba huo utaisaidia mamlaka hiyo kukabiliana na mapungufu yaliyoko.

# Msalala wataka elimu ya lishe bora

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga wamesema ma kukosekana kwa elimu ya mpangilio wa mlo katika familia zao chanzo cha utapiamlo kwa watoto.

Wamebainisha hayo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe kuhusiana na tatizo hilo kutokana na watoto kukosa lishe bora.

Walisema licha ya kulima mazao ya biashara na chakula kwa wingi na kupata fedha baada ya mauzo, juhudi hizo bure kutokana na kuendelea kuwapo kwa tatizo hilo.

Alisisitiza kuwa elimu hiyo ya namna ya kuandaa vyakula inatakiwa kusisitizwa katika jamii na hasa kwa wajawazito wanapokwenda kliniki ili kukabiliana na tatizo la utapiamlo kwa watoto kutokana na lishe duni.

Mkazi wa Segese, Rahma Abdul, alisema wanazalisha vyakula shambani, lakini hawafahamu namna ya kuandaa chenye lishe na kulazimika kula bila mpangilio.

Salvatori Wambura, alitaka elimu ya lishe ipewe kipaumbele kwa wanawake, wanaume na vijana wenye umri wa kuoa na kuolewa.

Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Peter Ngazo, alisema mtoto asipopata lishe bora anakosa uwezo wa kutunza kumbukumbu kwa kile anachofanyiwa au kuelekezwa.

Ngazo, alisema watahakikisha wanawafikia kinababa na vijana na kuwapa elimu ya makundi ya vyakula vyenye lishe ili wawahimize wenza wao namna ya kuandaa.

Alitaja vyakula vinavyotakiwa katika mlo kila siku kuwa ni vya makundi ya mafuta, matunda, asili ya wanyama, jamii ya mikunde, mbogamboga, nafaka, mizizi na ndizi mbichi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Rose Manumba, alisema wametenga Sh. milioni 78 kutoka mapato ya ndani ya kwa ajili ya kukabiliana na lishe duni kwa watoto chini ya miaka mitano na wajawazito.

"Mtoto anatakiwa kupata vyakula vyenye lishe, tunalima sana mazao ya chakula na biashara lakini hatufahamu namna ya kuandaa vyakula na kusababisha kuwa na watoto wenye utapiamlo," alisema Manumba na kusisitiza kuwa:

"Kumbukeni hata mjamzito anatakiwa kula vyakula vyenye lishe ili ajifungue mtoto mwenye afya."



Ukurasa 12

**Tume Madini na undani wa alichonadi Rais kununuliwa mashine mpya, Pato Taifa zaidi**




Ukurasa 13


Biashara chuma chakavu imejaa hujuma, hatari ya miundombinu

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 8, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**Hatima ya biashara na uwekezaji Afrika anaporejea Rais Trump**

MIAKA 58 CHAMA TAWALA...

# Botswana; falsafa na siasa za uchumi wa almasi zatawala kupindua meza

• Mteule; Mkomunisti anayekiri ugumu, umma wamkubali...

**Na Christina Mwakangale**

WIKI za hivi karibuni zinafuatana na simulizi zenye mtikiso utokanao na uchaguzi kitaifa, pia matokeo yake.

Kulianza Msumbiji, Frelimo ikaendelea kukalia kiti Msumbiji baada ya mchuano mkali, katika safari kuelekea miaka 50, matokeo yakapokewa na fujo za wapinzani, Renamo waliowahi kuwa wapiganaji porini.

Nchini Botswana, mwenyeji wa Ikulu miaka 58 tangu uhuru akang'oka wiki iliyopita, akiahidi kukabidhi nchi kwa amani na akatekeleza hivyo.


Wakati mada na mshangao huo haujaisha, ukatekwa na mwingine wiki hii, mchuano mkali wa Donald Trump kurudi Ikulu baada ya kukaa 'benchi' na mlolongo wa kashfa kipindi kimoja, akimteka fursa mwanamama Kamala Harris, aliyetaka kuweka historia ya kijinsia katika nafasi hiyo nchini Marekani.

Daima, mzizi wa uwekezaji kisiasa kote huko haujawahi kuwa mbali na matakwa ya siasa uchumi.

### KILICHOJIRI BOTWSANA

Nchi hiyo ilipata uhuru wake kutoka kwa Uingereza mnamo Septemba 30, 1966 sasa ina idadi ya watu ni milioni 2,675. Hao katika hesabu ya haraka ni sawa na nusu ya wakazi wa Dar es Salaam.

Ni nchi inayofahamika kwa ustawi na uthabiti kiuchumi muda mrefu, hasa kutokana na utajiri wa almasi, huku ikiwa na idadi ndogo ya watu wanaopewa huduma za bure kama elimu na afya.



Siku Rais wa Botswana, Mokgweetsi Masisi (kulia), alipopeana mkono wa kutakiana heri ya kukabidhiana ofisi na mteule wake, Duma Boko, mnamo Novemba 4, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, kushuka kwa bei ya almasi kwenye soko la kimataifa katika miaka ya karibuni, kunatajwa kuchangia kushuka mapato ya ndani, hata nchi hiyo sasa inaangalia sekta mbadala iwekeze.

Muda mfupi kabla ya uchaguzi mwisho wa mwezi uliopita, Rais wa Botswana anayeondoka madarakani, Mokgweetsi Masisi kutoka chama tawala- Botswana Democratic Party, akakiri almasi za nchi 'zilidoda' sokoni tangu mwezi Aprili mwaka huu, hata kuathiri uchumi wao.

### MASISI AKIWA UN

Mnamo Septemba mwaka 2022, Rais Masisi, akahutubia mjadala Mkuu wa Mkutano wa 77 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA77), akigusia mchango wa almasi katika uchumi wa Botswana.

Hapo akawa na ufafanuzi namna taifa hilo, limevuka kutoka umaskini hadi kuwa nchi ya kipato cha kati.

Masisi akawaambia viongozi wenzake kuwa:

"Hii ni hadhi ambayo tunajivunia nayo, kwa sababu tulipopata uhuru miaka 56 iliyopita (sasa 58), tulikuwa miongoni mwa nchi maskini zaidi duniani.

"Lakini tulibahatika kubaini kile kilichobainika hivi sasa duniani kuwa (Botswana), ni hifadhi kubwa zaidi ya machimbo ya madini ya almasi kwenye ukanda wa Kimberley."

Akawasifu viongozi watangulizi walioweka msingi mzuri wa kusimamia almasi yao, hapo nako akiwa na nukuu: "Viongozi wetu waliotangulia walichagua kugeuza simulizi ya kuwa na madini ya almasi kuwa simulizi ya maendeleo."

Masisi akafafanua kwamba, Botswana isingefika iliko kimaendeleo, pasipo kuangaliwa, kulindwa, kutetewa na misingi ya demokrasia iliyojikita kwenye utawala wa sheria na utawala bora, pia ulinzi wa haki za binadamu kwa watu wake.

Hata hivyo, timu ya wanasiasa wa upinzani wakiongozwa na muungano wao chini ya mkusanyiko uitwao Umbrella for Democratic Change (UDC) au 'mwamvuli wa mabadiliko ya kidemokrasia' BDP, wamekuwa wakikikosoa chama tawala kubaki madarakani muda mrefu.

Hiyo wanaitaja inachangia kuvuruga uchumi wao, pia kuwapo ufisadi, madai ambayo Masisi alikanusha, wakati huo akiwa Rais.

Masisi katika uwasilisho wake, akaipongeza ajenda ya mwaka 2021, iliyozinduliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres.

Mkuu huyo wa UN, akasema Botswana inazingatia kwa makini kuhakikisha rasilimali yake adhimu ya almasi inatumiwa kwa maslahi na maendeleo endelevu kwa wananchi wake.

"Nakumbusha chombo hiki adhimu kuwa simulizi ya Botswana ni ushahidi usio na shaka na ulio hai ya kwamba almasi ikisimamiwa vizuri ni kwa maendeleo. Ni kwamba almasi ni suala makini la kujipatia kipato," akatamka Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Rais Masisi, hata hivyo akakiri

**INAENDELEA UK.14**

UCHUMI

# Tume Madini na undani wa alichonadi Rais kununuliwa mashine mpya, Pato Taifa zaidi

## • Simulizi namna mauzo na makusanyo yanapaa…

**Na Mwandishi Wetu**

NI wiki mbili na nusu zimepita, tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aatamke kuhusu uwekezaji wa kisasa katika uchimbaji madini, kwa kuletwa mitambo ya kisasa itakayoiboresha izalishe zaidi.

Hapo akasisitiza matumizi ya madini kubaki sura chanda na pete kisera na miongozo ya nchi, akinena: "Mitambo hii ikifika nchini itagawanywa pote. Ila nimemtaka Waziri (Anthony Mavunde - Madini), atenge mitambo miwili kwa ajili ya vijana na mmoja wanawake."

Kauli ya Rais Dk. Samia, ni mwendelezo wa dhamira ya serikali yake kusukuma Sekta ya Madini nchini inaendelea kuongeza mchango ukuaji wake kiuchumi, kuchangia asilimia 10 au zaidi ya Pato la Taifa ifikapo mwakani.

Hadi sasa inaelezwa mitambo mitano imewasili nchini na 10 iko njiani kurahisishia wachimbaji wadogo kupata taarifa za uchimbaji na kuwanusuru na hasara.

Inaelezwa, sehemu ya manufaa yake inawanusuru wadau husika kulanguliwa na hadi sasa, takwimu kitaifa zinarejea kipindi cha miaka mitatu na nusu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, kumekuwapo maboresho ya ukuaji sekta ya madini nchini.

Hiyo inatajwa kuongezeka kutoka asilimia 9.4 ya uchumi wa nchi mwaka 2021 hadi asilimia 11.3 za mwaka jana.



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo alipotembelea soko la madini mkoani Geita, hivi karibuni. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

### TUME YA MADINI

Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Mhandisi Ramadhani Lwamo, anafafanua ni matokeo ya maboresho ya sheria husika, kanuni na miundombinu husika, ikiwamo umeme migodini katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Samia.

Anasema, kati ya mwaka 2021 hadi 2023, kampuni hizo zilizalisha ajira 19,356, kati yake 18,853 ni za Watanzania, sawa na asilimia 97.40, huku wageni wako 503 sawa na asilimia 2.60 ya ajira hizo mpya.

Lwamo anasema, hilo linaendana na kuwapo bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani 3,780,161,183.28 zilizouzwa na kusambazwa kwenye migodi mbalimbali nchini.

Katika orodha yake, kampuni za Watanzania ziliuza bidhaa za thamani ya Dola za Marekani 3,465,592,451.28 sawa na asilimia 91.68 ya mauzo tajwa na na huduma zilizotolewa migodini.

> **Masoko haya yamesaidia kuongeza mapato ya serikali kupitia tozo na ada zinazotozwa kwenye masoko haya.**

### MAKUSANYO JUU

Mhandisi Lwamo anasema maboresho ya sheria, kanuni na miundombinu ikiwamo ya umeme migodini ndani ya miaka mitatu ya mikakati na uongozi wa Rais Dk. Samia kupitia Tume ya Madini, makusanyo ya maduhuli ya serikali migodini yamepanda kutoka shilingi bilioni 624.61 za Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi shilingi bilioni 753.82 za mwaka uliopita, 2023/24.

Hapo anafafanua kwamba makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 20.7 kwa miaka mitatu iliyopita.

"Mathalan, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 tulipewa lengo la kukusanya shilingi trilioni moja. Hadi kufikia Oktoba 21 mwaka huu, Tume ya Madini imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 312.75 sawa na asilimia 31.28 ya lengo la mwaka," anasema Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini.

Lwamo anawaambia wahariri wa vyombo vya habari mjini Dar es Salaam kwamba, Pato la Taifa mwaka 2021 kwa madini iliingiza asilimia 7.2, huku mwaka jana ikapanda kufika asilimia tisa, kutokana na kuimarika usimamizi wa shughuli zake nchini.



Wachmbaji wadogo wakiwa kazini, wakitumia stadi za asili.

### MWELEKEO KISEKTA

Lwamo anasema, mwelekeo wa sekta kuchangia Pato la Taifa inadhamiria kuzidi asilimia 10 mwaka 2025, kama inavyofafanuliwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2020 na Tume ya Madini wa Mwaka 2024/25, hadi 2025/26.

Anasema, tume hiyo ina mikakati endelevu inayoimarisha usimamizi na udhibiti wa maeneo ya uzalishaji madini, ujenzi na madini ya viwandani.

Hilo analitaja linaongezewa na Wakaguzi Wasaidizi wa Madini Ujenzi (AMA), vitendea kazi na kushirikisha mamlaka nyinginezo za serikali zinazosimamia rasilimali hizo, ili kuongeza makusanyo na rasilimali yanayotokana na madini, pia ujenzi na mifumo na viwanda vya madini.

Anataja ushirikiano wa vyombo vya kiserikali; halmashauri zilizopo, Polisi, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) zimechangia kupigwa hatua hizo.

Lwamo anaataja mkakati mwingine ni kudhibiti biashara haramu za madini, hususan utoroshaji, serikali ikihamasisha utumiaji masoko na vituo vya madini nchini.

Pia anataja kuimarishwa vituo vya ukaguzi mipakani, bandarini na viwanja vya ndege, ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi na mapato.

Hilo linaendana na maboresho na usimamizi wa mfumo wa utoaji leseni za madini, kupunguza migogoro itokanayo na mwingiliano wa maombi ya leseni, muda wa utoaji huduma na kuongeza idadi ya leseni kila mwaka, wakihamasisha uwekezaji zaidi.

Lwamo pia anataja kuimarishwa ukaguzi wa uchimbaji migodini, lengo ni kuwa na uchimbaji endelevu ulio salama, ikiwamo kiafya na mazingira, ikiongezwa mapato, kuimarisha uchimbaji endelevu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Lwamo, anasema kwa kuimarisha Ofisi za Maofisa Madini Wakazi wa Mikoa (RMO) na maabara katika maeneo ya uzalishaji nchini, kutasogeza huduma karibu na wadau, hivyo kuchochea uwekezaji utakaowezesha serikali kuongeza mapato yatokanayo na madini.

Mikakati mingine inajumuisha kuimarishwa utafiti wa kutambua vyanzo vipya vya mapato ya madini na kuiwezesha tume kuongeza wigo wa makusanyo yake, ikiimarisha uwekezaji kwa wachimbaji, ajira zao na sekta endelevu.

### MAUZO YANAPAA

Lwamo anasema kupitia Wizara ya Madini, tume hiyo kwa kushirikiana na Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nchini, imeendelea kusimamia utendaji kazi wa masoko ya madini na vituo vya ununuzi.

"Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 mauzo ya madini katika masoko na vituo vya ununuzi wa madini yalikuwa Shilingi bilioni 2,592.02 na mapato yaliyopatikana kutokana na mauzo hayo ni kiasi cha shilingi bilioni 180.13 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22 ambapo ilikuwa shilingi bilioni 2,361.80.

"Mapato ya Serikali yaliyopatikana ni shilingi bilioni 164.09, yalihusisha mrabaha na ada ya ukaguzi wa madini nchini," anasema Lwamo.

### WATANZANIA KUNUFAIKA

Lwamo anasema tume yake inahakikisha wananchi wananufaika, ikiendelea kusimamia na kuwasilisha mipango ya ushirikishwaji kisekta kutoka kwa wamiliki, waombaji leseni za madini na watoa huduma, kwa mujibu wa sheria inavyowaelekeza.

Anarejea kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023, wamewasilisha mipango 1,050 ya ushirikishwaji wananchi katika sekta hiyo na 1,036 ilikidhi vigezo, 14 pekee haikukidhi na kwa marekebisho.

Kwa mujibu wa Lwamo, tume katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2023, kampuni za madini zilizalisha ajira 19,356, kati yake, 18,853 ni Watanzania sawa na asilimia 97.40 na 503 wageni asilimia 2.60 ya ajira hizo zilizozalishwa.

Anasema bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani 3,780,161,183.28 ziliuzwa na kusambazwa kwenye migodi mbalimbali nchini.

Kati yake kampuni za nchini ziliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani 3,465,592,451.28 sawa na asilimia 91.68 ya mauzo yote na huduma zilizotolewa migodini.

Hiyo ikaendana na kutolewa 34,348 sawa na asilimia 92.04 zilizopangwa kutolewa, akizitaja leseni hizo ni za uchimbaji mkubwa, kati, mdogo, biashara ya madini na uchenjuaji wake.

### KUDHIBITI UTOROSHAJI

Lwamo anasema kuanzishwa masoko ya madini nchini, kumedhibiti utoroshaji madini na kuongeza uwazi katika sekta hiyo.

Anasema hadi sasa kuna masoko 44 na vituo 106 vidogo vya ununuzi wa madini vimeanzishwa nchini, pia kudhibiti bei zake kwa kutolewa bei elekezi shindani, ikilinganishwa na soko la dunia.

"Masoko haya yamesaidia kuweka mifumo ya kufuatilia na kusimamia biashara ya madini, ikiwamo teknolojia za kidijitali kusaidia kurekodi taarifa za madini kutoka kwa wachimbaji hadi kwa wanunuzi," anasema Lwamo.

"Masoko haya yamesaidia kuongeza mapato ya serikali kupitia tozo na ada zinazotozwa kwenye masoko haya," anafafanua.

### MINADA YARUDISHWA

Akizungumzia minada, Lwamo anasema serikali kupitia tume inatarajia kurejesha minada ya ndani ya madini ya vito katika maeneo ya uzalishaji.


Maeneo hayo ni pamoja na Mirerani, Mahenge, Tunduru, Dar es Salaam, Arusha na Tanga na ya kimataifa katika mji wa Bangkok na Jaipur nchini India.

"Uendeshaji wa minada hii ni fursa muhimu ya kutangaza madini ya vito vinavyozalishwa nchini hususan kwenye masoko ya kimataifa," anasema.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Biashara chuma chakavu imejaa hujuma, hatari ya miundombinu




**Na Sabato Kasika**

BIASHARA ya vyuma chakavu imeenea karibu kila kona ya nchi, watu wanajitafutia riziki kwa kutafuta vyuma hivyo, kuvikusanya na kwenda kuviuza ili wajipatie fedha kwa ajili ya matumizi yao ya kila siku.

Hata hivyo, ninadhani biashara hiyo inapaswa kumulikwa, kwani baadhi ya watu wanaokusanya vyuma hivyo chakavu, wanaharibu na kuiba miundombinu mbalimbali ikiwamo ya barabara.

Kwa mfano, unaweza kukuta pembeni mwa kingo za madaraja kumefungwa vyuma, lakini baadhi ya watu wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha kuvifungua na kwenda kuviuza kama chuma chakavu.

Wakati vyuma hivyo viking'olewa, wengine wanachukua mifuniko ya chemba za maji ya mvua na kwenda kuiuza kama chuma chakavu, kitendo ambacho ni wazi kuwa ni hujuma.

Biashara ya ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi na urejelezaji wa chuma chakavu si mbaya, kwani kwa namna moja au nyingine unasaidia kutunza mazingira, lakini inapofikia kuharibu miundombinu, ninadhani unageuka kuwa hujuma, hivyo wenye mchezo huo wangemulikwa.

Ni vyema wanaofanya biashara ya chuma chakavu wasiwe chanzo cha uharibifu wa miundombinu ya barabara na maeneo mengine, kwani uharibifu huo sasa umesababisha kusiwapo mifuniko ya chuma kwenye chemba za maji ya mvua katika baadhi ya maeneo.

Limekuwa jambo la kawaida kukuta mfuniko umeondolewa na badala yake limewekwa gurudumu au matawi ya miti kama ishara ya kuwatambulisha madereva kuwa kuna shimo mbele.

Hujuma za aina hiyo, ninadhani ndizo zimesababisha hata mkandarasi anayepanua Barabara ya Morogoro kuanzia Kimara hadi Ubungo, Dar es Salaam kuamua kuweka mifuniko ya zege kwenye chemba mpya.

Ninadhani ni wakati sasa wafanyabiashara wa chuma chakavu kuwa waaminifu na kuepuka kujihusisha kuhujumu miundombinu. Wafanye kazi na serikali kwa kuwafichua wanaoharibu miundombinu na kuiuza kama chuma chakavu, kwani kitendo hicho ni sawa na uhujumu uchumi.

Binafsi ninaamini kwamba mtu akifanya biashara yake kwa kufuata taratibu, hawezi kujihusisha na hujuma. Hivyo, hata wanaokusanya chuma chakavu kutoka kwa watu mbalimbali, wangekuwa makini.

Katika maisha ya sasa, kuna baadhi ya watu wapo tayari kufanya hujuma ili wajipatie fedha, wafanyabiashara wanatakiwa kuwa makini na watu wa aina hiyo ili wasiwaingize katika mtego.

Biashara hiyo imeongeza ajira kwa baadhi ya vijana wanaopita mitaani na kuokota vyuma hivyo, lakini inawezekana wapo baadhi ambao wanajihusisha na wizi wa miundombinu na kuiuza kama chuma chakavu.

Kwa hiyo, wafanyabiashara wa chuma chakavu wangejihadhari na ununuzi wa vyuma vinatokana na miundombinu ya serikali, kwani wanaowapa vyuma hivyo wapo tayari kufanya hujuma wapate fedha.

Yapo baadhi ya maeneo, wameiba hadi vibati vya anuani za makazi na kwenda kuiuza kama chuma chakavu. Yote hayo ni hujuma na kuharibu kodi za wananchi zilizotumika kutengeneza vibati hivyo.

Inasikitisha kuona ujenzi wa barabara umekamilika na miundombinu yake, lakini baada ya muda mfupi, mifuniko ya chemba za maji ya mvua haipo au vyuma vya kingo za barabara vimeng'olewa.

Huo sio uzalendo. Kama tunashindwa kulinda miundombinu yetu tunataka aje nani atulindie? Hapa kuna tatizo la ukosefu wa uzalendo kwa kushindwa kulinda na kuthamini vitu vyetu.

Tutafakari kisha tuchukue hatua, kwani hakuna mtu kutoka nje atakayekuja kulindia miundombinu bali ni sisi Watanzania wenyewe, ingawa wengine huwa wanasema hiyo ni mali ya umma au haina mwenyewe.

Mawazo hayo ndio yanayosababisha hata tunapoona hujuma zinafanyika, hatuchukui hatua zozote za kuhakikisha tunazuia, badala tunaona ni jambo la kawaida kukuta mifuniko ya chemba katika barabara imeibiwa huku kukiwa kumefunikwa na gurudumu au majani.

BIASHARA

# Hatima ya biashara na uwekezaji Afrika anaporejea Rais Trump

**Na Mwandishi Wetu**

• Kitendawili cha AGOA kuendelea kuwapo

UTAWALA unaoondoka wa Rais Joe Biden unatajwa ulijaribu kujenga hisia kwamba, Afrika ilikuwa mshirika wa thamani na muhimu," anavyotamka W Gyude Moore, mshirika katika Kituo cha Maendeleo ya Dunia na waziri wa zamani wa Liberia.

Inaelezwa, msatafu Rais Biden, alijitahidi kupatanisha shauku hiyo na mikataba na ushirikiano mkubwa, lakini hiyo haimaanishi kuwa mkakati wake wa Afrika haukuwa na matunda.

Marekani ilisifiwa kwa kuwekeza katika Ukanda wa Lobito - njia ya reli inayopitia Angola, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Zambia, ambayo itatumika kusafirisha malighafi muhimu.

Mnamo mwaka 2023, Marekani ikasema imewekeza zaidi ya Dola za Marekani bilioni 22 tangu Biden aingie madarakani.

Lakini kuna wasiwasi kwamba ujio wa Rais Trump, anaweza kuondoa uwekezaji na biashara hii. Rais wa hivi karibuni ana mtazamo wa kulinda zaidi maslahi ya nchi yake, usio wa kawaida kuliko Biden.

Mkataba wa Ukuaji na Fursa ya Afrika (AGOA), ambao umewezesha nchi zinazostahiki za Afrika kuuza nje baadhi ya mazao yao kwenda Marekani bila kulipa kodi tangu mwaka 2000, unatajwa chanzo kikuu cha wasiwasi huo.



Rais Donald Trump. **PICHA: MAKTABA**

Wakati wa utawala wake uliopita, Trump alisema mpango huo hautaongezwa muda wakati utakapoisha mnamo 2025.

Na wakati wa kampeni yake ya 2024 aliahidi kutekeleza ushuru wa mapato wa asilimia 10 kwa bidhaa zote zinazotengenezwa na nchi za kigeni.

Hiyo inaelezwa kwamba itafanya bidhaa zinazoagizwa kuwa ghali zaidi na hivyo wauzaji nje ya Afrika watakuwa na uwezekano wa kuuza mazao yao kidogo katika soko kubwa la Marekani.

Wachambuzi wengi nchini Afrika Kusini - mmoja wa wauzaji bidhaa nje wakubwa chini ya mkataba wa AGOA - wametabiri kuwa kukata mkataba wa AGOA kunaweza kuwa na athari kubwa katika uchumi.

Hata hivyo, taasisi ya ushauri ya Marekani ya Brookings inatabiri kuwa Pato la Taifa la Afrika Kusini litapungua kwa "asilimia 0.06 pekee". Hiyo kwa kiasi fulani ni kutokana na kwamba bidhaa nyingi ambazo Afrika Kusini inauza nje kwenda Marekani kama vile madini na chuma hazifaidiki na Agoa, ilisema.

Ingawa Rais Donald Trump hakutaka AGOA, alitambua kwamba ikiwa Marekani itakabiliana na ongezeko la ushawishi wa kiuchumi wa China barani Afrika, ilihitaji kudumisha kiwango fulani cha ushirikiano.

Mwaka 2018 utawala wa Trump ulizindua Prosper Africa - mpango ambao unasaidia kampuni za Marekani zinazotaka kuwekeza Afrika na Shirika la Fedha la Maendeleo (DFC).

Ni shirika linalofadhili miradi ya maendeleo barani Afrika na duniani kote. Biden ameendelea kuuendesha baada ya kuchukua wadhifa wake na DFC inasema hadi sasa imewekeza zaidi ya Dola za Marekani bilioni 10 barani Afrika.

Ikizingatiwa kuwa China bado ina nguvu kubwa barani Afrika na kwamba Trump alianzisha sera hizo mwenyewe, kuna uwezekano mkubwa wa kufikiria mara mbili kabla ya kuzipunguza.

• *Kwa mujibu wa BBC*

## Botswana; falsafa na siasa za uchumi wa almasi zatawala kupindua

**INATOKA UK.11**

namna wanavyopata changamoto kwenye kuvutia wawekezaji, kusaidia kupanua wigo wa sekta ya uchumi. Akaahidi kutumia kila jukwaa kusaka wawekezaji kwenye sekta nyinginezo.

**DAI LA AJIRA UN**

Mokgweetsi Masisi, katika hotuba yake hiyo kwenye mjadala, akasema marekebisho yoyote ya muundo wa Umoja wa Mataifa (UN), yatakuwa na maana kwa mataifa madogo kama Botswana, pale yatakaporuhusu kila nchi kushiriki kwa usawa bila kujali ukubwa wao.

"Mimi na serikali yangu tuna hamu ya kuona wananchi wetu wakiwakilishwa na wakiajiriwa ndani ya mfumo wa UN na kwa urais wetu wa Baraza la Uchumi na Kijamii, ECOSOC.

"Naamini Botswana imeonyesha uwezo wake, ikiwamo vijana wetu ambao wamepatiwa tathmini nzuri kutokana na usaidizi wao kwa Sekretarieti ya ECOSOC wakati wa awamu yetu," akasema.

**DIRA YA MTEULE**

Huyo ni mwanasheria, Duma Boko (55), anayetasfsiriwa kisiasa mwenye kujiamini, pia ana maadili mema, huku akiwa na sifa ya kutohofia jambo.

Kitaaluma alipata elimu ya sheria nchini mwake, kisha akainakishi kitaaluma katika Shule ya Sheria ya Havard, Marekani na sasa ni mbobevu katika haki za binadamu.

Katika kijiti alichopokea, anatajwa kuwa na 'kibarua kigumu' kuimarisha uchumi wa nchi, pia wananchi wake 'wanamkodolea macho' hatima ya maslahi yao.

Elimu yake ya uanasheria ilianzia nchini mwake, hatimaye kwenda Shule Kuu ya Sheria Harvard, huko Marekani.

Hata hivyo, kisiasa ushindi wake, umeushangaza umma na dunia, kutokana na kuvunja dhana 'wapinzani Botswana hawawezekani...'

Kwa miaka 50 upinzani wa kisiasa nchini humo, wamekuwa wakiota ndoto, kukivua madaraka chama kikuu cha Botswana Democratic Party, lakini ni Boko pekee ndiye aliyefanikisha hilo.

Maoni ya kwanza akatoa Ijumaa iliyopita, kwamba anatamka: "Ninaweza tu kuahidi (kwa watu) nitafanya kila niwezalo. Nitakaposhindwa, nitawatazama wao, waniongoze."

Rais Boko anabainisha nchi hiyo inakopita ni changamoto za kiuchumi an anahidi kuleta mabadiliko katika ajira na mishahara serikalini.

Mbinu zake kwenye kampeni zilimbeba.

Katika muda wote wa kampeni yake, mikutano ya hadhara, Boko akawaomba wafuasi wake kuja karibu awasikilize malalamiko yao, hali iliyoonekana kuwavutia vijana.

Rais Boko, awali alikataa kuwania nafasi ya ubunge kama alivyoshauriwa, akahamisha ujasiri kuwania urais, ambako kampeni zake zilionyesha mafanikio ya awali, kutokana na kuvutia hadhira na kuwa rafiki yao.

Mzaliwa huyo wa mwaka 1969, katika mji mdogo wa Mahalapye, safari yake iliyoanzia kuongoza baraza la wanafunzi, badaaye akaibuka kuwa mwanasheria maarufu nchini, mwake, kwa mujibu wa mchambuzi wa kisiasa, Lesole Machacha.

Kisiasa, baadaye akawa kiongozi wa Chama cha Kitaifa cha Botswana (BNF) mwaka 2010, kilichotajwa kuwa na "itikadi za kikomunisti" ana kuna wakati akaongoza katika mgogoro na wahadhiri katika chuo kikuu alichofundishja akiwaambia 'hawafai.'

Baada ya kutangazwa kushindwa wiki iliyopita, Rais Masisi kama alivyofanya Mama Harris Marekani wiki hii, akatamka ameshazungumza na kiongozi wa chama cha upinzani cha mrengo wa kushoto - UDC, Duma Boko, kupanga namna ya kukabidhi madaraka.

Zaidi ya watu milioni moja walijiandikisha kupiga kura katika uchaguzi huo kati ya raia milioni 2.6 wa taifa hilo.

Ni ni mara ya tatu kwa Boko kuwania nafasi ya urais na baada ya matokeo ya awali kupitia ukurasa wake wa 'Facebook' kiongozi huyo wa upinzani akandika "mabadiliko yamewadia."

**Kwa msaada wa mtandao**



# Mbunge: SGR isafirishe mizigo

Na Augusta Njoji, DODOMA

MBUNGE wa Ole (CCM), Juma Hamad Omar, ameshauri treni ya reli ya kisasa (SGR) kuharakisha usafirishaji wa mizigo ili kurejesha fedha zilizowekezwa na serikali.

Wito huo ni kati ya hoja zilizoibuliwa kwenye mjadala wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2025/26.

Akichangia mapendekezo hayo bungeni jana, Omar, alisema SGR ni mkombozi mkubwa, lakini bado inasafirisha abiria na si mizigo.

"Lazima SGR ijikite pia katika usafirishaji wa mizigo, kama hii reli inachukua watu itachukua muda mrefu kufikisha kiasi cha fedha kilichowekezwa na ili tuone manufaa inabidi tuharakishe kuanza kusafirisha mizigo," alisema na kuongeza:

"Ulaya reli ni ya serikali, mabehewa ni ubia, hivyo tuipe nafasi sekta binafsi ishiriki katika reli ibebe mizigo. Pia nashauri vipande vilivyobaki vya kujenga serikali isibebe mzigo kuna haja ya kwenda PPP."

Kuhusu nishati, alisema kuna upotevu wa umeme kwa kiwango cha asilimia 14, hivyo ni muhimu kubadili miundombinu kwa kuwa iliyoko ni chakavu.

Mbunge wa Mpanda Vijijini (CCM), Selemani Kakoso, alisema ili kutengeneza uchumi kutokana na uwekezaji unaofanyika kwenye SGR ni lazima kuwe na mikakati ya kujenga misingi ya kuhodhi uchumi wa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC).

"Uchumi lazima uende kuwekeza nchi nyingine ili uvute kwako na hata kwa Uganda unganisha treni ya Dar es Salaam hadi Mwanza kuwe na mkakati wa kupeleka mzigo mikubwa sana kwenda Uganda tofauti na sasa ambayo ni asilimia kama tano ndiyo mzigo kwenda nchi hiyo," alisema.

**"Ulaya reli ni ya serikali, mabehewa ni ubia, hivyo tuipe nafasi sekta binafsi ishiriki katika reli ibebe mizigo. Pia nashauri vipande vilivyobaki vya kujenga serikali isibebe..."**

### WATUMISHI VIJIJINI

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janejelly Ntate, alisema kuna ombwe la kutopanga vizuri rasilimali watu na mgawanyiko usio sahihi wa watumishi.

Janejelly, aliishauri serikali kuweka motisha ili kuwavutia watumishi wa umma kukaa vijijini na wilaya za pembezoni mwa nchi wanazopangiwa.

"Hawataki kukaa vijijini na kwenye wilaya za pembezoni, serikali kuna kitu mnatakiwa mkiangalie kwa kuweka incentives, kuna haja ya kuzirudisha kwa ajili ya walio vijijini, na tuweke utaratibu akiwa kule sheria izingatiwe akae kituo cha kazi miaka mitatu," alisema.

Alishauri iundwe kamati kuangalia matumizi ya serikali ili yawe sawa.

"Kwa mfano kuna kitu kimoja lakini kinafanywa na wizara tatu, yaani kilimo wanachimba mabwawa yale yale yakatumiwa na mifugo na Wizara ya Maji, hapa bajeti itakuwa imetumika kidogo kuliko sasa kila wizara ina fedha za kujenga mabwawa," alisema.

### ARDHI TISHIO

Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya alisema suala la ardhi linaanza kuwa tishio kwa kukosa mipango mizuri.

"Ardhi iko kwa Watanzania na Rais ni msimamizi mkuu, lakini hii nchi ina watu wengi wanaokuja kutoka nje na kuchukua maeneo ya kutosha kwa kisingizio cha uwekezaji. Watanzania wanaiangalia ardhi itafika wakati hawatakuwa na ardhi," alitahadharisha Manyanya.

Alishauri ufanyike mpango wa kutosha ili kundi la vijana lisaidiwe kupata ardhi kwa utaratibu wa kuwezeshwa.



Mbunge wa Kibaha Mjini mkoani Pwani, Sylvester Koka (kulia), akizungumza na wageni wake, walimu kutoka jimboni mwake, waliomtembelea bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watakiwa kumuunga mkono Rais Samia

Na Paul Mabeja, DODOMA

WADAU nchini wametakiwa kuunga mkono juhudi za kukuza usawa wa kijinsia nchini zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Wito huo ulitolewa juzi jijini hapa na Mshauri wa Rais na Mwenyekiti wa Kamati ya Jukwaa la Kizazi chenye Usawa, Angellah Kairuki, kwenye hafla ya uzinduzi wa kitabu ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia kwenye masuala ya usawa wa kijinsia.

"Wanawake hawapaswi kukaa bure serikali hii iliyopo madarakani imetoa fursa nyingi waendelee kuzitumia ili kujikwamua kiuchumi," alisema.

Alisema Rais Samia amekuwa akitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii na uchumi kwa wanawake ili waondokane na umaskini.

Kairuki, alisema kwenye eneo la usawa wa kijinsia, amekuwa akihakikisha hakuna anayeachwa nyuma.

Mwandishi wa kitabu hicho, Mwanasheria na Mhadhiri Msaidizi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI), Penina Manyanki, alisema ni maalum kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais Samia kwenye masuala ya kizazi chenye usawa.

Vilevile, alisema malengo ya kitabu hicho ni kutoa uelewa wa kisheria kuhusu haki za wanawake na nafasi ya mahakama za Tanzania kuzilinda.

"Nimezungumzia sera na mipango mikakati ya programu za kitaifa kukuza usawa wa kijinsia nchini, nafasi za serikali kuu, mitaa, taasisi za fedha, mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuwezesha wanawake na kukuza usawa wa kijinsia nchini.

"Kitabu hiki ni 'special dedication' kwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za kiuchumi hususan kwa wanawake," alisema.

Alisema katika kipindi chake cha uongozi Samia amekuwa akitoa fursa ili wanawake wajiinue kiuchumi na kuwa na neema katika familia na jamii.

# Wizara ya Maji yaipa RUWASA magari

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

WIZARA ya Maji imetoa magari matano yenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 795 kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoani hapa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya sekta ya maji.

Magari hayo yalikabidhiwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego kwa ajili ya Wilaya ya Singida Mjini, Manyoni na Kiomboi, RUWASA Mkoa wa Singida na RUWASA Wilaya ya Iramba.

Meneja wa RUWASA wa Mkoa huo, Lucas Said, alisema magari hayo yametolewa ili kuhakikisha mamlaka hiyo inatatua kero za maji mkoani humo.

"Kama unavyofahamu tunaendelea kufanya kazi kuhakikisha tunafikia malengo ya kufikia asilimia 85 vijijini na mijini asilimia 95 ifikapo Desemba 2025, " alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Sebastian Warioba, alisema watahakikisha wanafikia malengo ya kufikisha maji kwa wananchi.

"Sisi watumishi wa sekta ya maji katika Mkoa wa Singida tunakuahidi tutaendelea kuchapa kazi kwa umoja, uadilifu na kujituma ili tuweze kufikia yale malengo, tunatoa shukrani kwa Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso wanavyotujari na kutusimamia kuhakikisha tunamtua ndoo mama kichwani," alisema.

Dendego, alisema kiwango cha upatikanaji wa maji kwa sasa kwa mkoa huo kimefikia asilimia 68.2 vijijini na asilimia 86 mjini.

"Kupewa magari haya tumeongezewa mwendo kasi na ari kuhakikisha miradi yetu tunayotekeleza iweze kutekelezwa kwa kasi kubwa ili kufikia malengo kabla ya muda uliopangwa," alisema.

Alisema Singida wamejiwekea malengo ikifika Juni 2025 uwe umepeleka asilimia 85 ya maji vijijini na 95 mjini yatakuwa yamefikiwa.

Alisema serikali imekuwa ikiendesha kampeni ya kumtua ndoo mama kichwani hivyo ili kufanikisha ni lazima kuwapo na vitendea kazi kama magari.



# Maambukizi Ukimwi tishio Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KIWANGO cha maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kimeongezeka kwa asilimia 0.6 katika Halmashauri ya mji Njombe kutoka asilimia 11.8 hadi asilimia 12.4, imeelezwa.

Imeelezwa kuwa vijana wa kuanzia umri wa miaka 15 hadi 49 ni kundi ambalo liko hatarini kukumbwa na maambukizi ya virusi hivyo katika halmashauri hiyo.

Hayo yalielezwa juzi wakati Mwenyekiti wa Kamati ya Ukimwi ya halmashauri hiyo, Nestory Mahenge akiwasilisha taarifa ya hali ya maambukizi hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, madiwani waliishauri serikali kuchukua hatua kwa kutoa elimu kuanzia shuleni hadi mtaani ili kukabiliana na maambukizi hayo kusambaa katika jamii.

Diwani wa Viti Maalum, Tumaini Mtewa, alisema umri wa miaka 15 watoto wanakuwa kwenye mihemko, ipo haja kwa kamati za Ukimwi kutoa elimu kuwanusuru na janga hilo.

**"Lengo letu CHADEMA ni kuhakikisha tunashinda uchaguzi wa serikali za mitaa kwa asilimia 95, hatupendi tushinde mitaa yote kwa kuwa tutakosa watu wa kutukosoa na tutafanya**

"Ukiangalia ni watoto ambao wako shule za sekondari, niombe elimu zianze kutolewa kuanzia shule za msingi ili kuhakikisha asilimia inashuka," alisema Tumaini.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Jabir Juma, alisema wameanza kuchukua hatua stahiki ikiwamo kuanzisha ATM za kinga katika maeneo mbalimbali ya mji huo.

"Vipimo vya sasa tunapima na kubaini huyu ameambukizwa kwa muda mfupi au kwa muda mrefu," alisema Dk. Juma.

Aliwataka vijana kuchukua tahadhari kwa kutumia kinga na kuacha tabia ya kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja ili kuepuka maambukizi ya Ukimwi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Mpete, aliagiza elimu ya Ukimwi kuendelea kutolewa kwa vijana kwa njia mbalimbali, ikiwamo michezo na kukosa muda wa kushiriki ngono zembe.



Kaimu Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Ileje, mkoani Songwe, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Raphael Magoma, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa dereva wa pikipiki ya magurudumu matatu baada ya kuzidisha mzigo na abiria juu, katika barabara ya Mpemba-Ileje jana. Magoma alitoa elimu na kuwachukulia hatua wasiozingatia sheria za usalama barabarani ili kudhibiti ajali. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

# Misitu yapaisha mapato halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Njombe mkoani Njombe imesema inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 3.5 kwa mwaka kutokana na mazao ya misitu na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Idara ya Misitu na Mazingira wa Halmashauri hiyo, Ahamad Maguo, wakati akikabidhi vyeti kwa wanafunzi wa klabu ya mazingira wa Shule ya Sekondari Ikuna. Maguo, alisema mapato hayo yanaisaidia halmashauri hiyo kutekeleza miradi hiyo ikiwamo ya elimu na afya.

Alitoa rai kwa wanafunzi na wakazi wa halmashauri hiyo kuthamini na kutunza mazingira ili kutimiza lengo la halmashauri hiyo la kukusanya mapato zaidi kutokana na mazao ya misitu. "Sisi tunategemea mapato yetu yanayotokana na mazao ya misitu, kwa hiyo watu watakapopanda miti katika halmashauri hii ikiwamo Kata ya Ikuna, Shule ya Sekondari Ikuna basi wewe mpandaji utapata mapato pamoja na halmashauri," alisema Maguo.

Baadhi ya walimu wa shule hiyo, akiwamo Benjamin Mpongano, alisema pia wanawafundisha wanafunzi kuandaa vitalu vya miti ili kukuza mapato ya shule.

Mwanafunzi, Andrew Msigwa, alisema pamoja na jitihada zao kutunza mazingira, wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji.

"Katika shule yetu tuna miti ambayo tumepanda wenyewe, tuna bustani ya mboga, lakini tatizo la maji wakati wa kiangazi linasababisha mimea kufa," alisema.

# Marufuku biashara njia ya waenda kwa miguu

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

UONGOZI wa umoja wa wafanyabiashara katika soko kuu la mjini hapa, umepiga marufuku biashara kufanyika kwenye njia ya waenda kwa miguu na kuwaonya watakaokiuka watachukuliwa hatua kali kwa kusababisha usumbufu kwa wateja.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Umoja huo, Oku Hongoli, wakati wa mkutano na wafanyabiashara hao wa kuhamasisha kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali.

"Sio mjadala yeyote atakayeona yupo kwenye njia kuu wanazopita watu natoa siku tatu biashara hizo zitolewe ili waweze kupita kwa uhuru na sio kuminyana minyana," alisema Hongoli.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuchangamkia fursa za serikali kukuza biashara, uchumi, kupata vitambulisho na kuwa walipakodi.

"Tuchangamkie fursa za serikali tusiwe wazembe kwenye hili kwa sababu imejitahidi kutatua changamoto zetu," alisema Hongoli.

Kaimu Meneja wa Soko hilo, Lusajo Mwakiluma, alisema utaratibu wa baadhi yao kufanya biashara umekuwa ukileta usumbufu kwa wateja, jambo ambalo halivumiliki.

"Sasa inafika hatua hata kupishana watu inakuwa ni ngumu na ndipo wizi unapoanzia," alisema Mwakiluma.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Chris Mlowe, alitaka kufahamu vigezo vya kupatiwa mikataba rasmi ya kuendelea kufanyabiashara kwa uhalali.

Mkazi wa mjini hapa, Sarah Tweve, alisema kumekuwa na usumbufu wakati wa kuingia sokoni kutokana na msongamano wa machinga. Sarah, aliushukuru uongozi wa wafanyabiashara hao kwa kuwa utasaidia kuondoa usumbufu na msongomano sokoni hapo.



## HABARI ZANZIBAR

# Vyombo vya habari kupewa tuzo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kinatarajia kutoa tuzo ya uwiano wa kijinsia kwa vyombo vya habari katika Maadhimisho ya Siku ya Redio Duniani.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za TAMWA visiwani hapa, Mkurugenzi wa chama hicho, Dk. Mzuri Issa alisema tuzo hiyo iliyopewa jina la "Kalamu yangu, mchango wangu kwa wanawake" itatolewa Februari mwakani.

Dk. Mzuri, alisema tuzo hiyo inatolewa ikiwa ni kutambua mchango wa vyombo vya habari na waandishi wa habari kuhusu mafanikio, changamoto, michango ya wanawake katika uongozi na kukuza usawa wa kijinsia kupitia kazi zao.

Alisema pia tuzo hiyo inatolewa ikiwa ni kuhamasisha vyombo vya habari na waandishi wa habari kuunga mkono sauti ya wanawake na kukuza uandishi wa habari wenye kuzingatia usawa wa kijinsia ili kuchangia mabadiliko ya kijamii.

"Huu ni msimu wa nne tangu tulipoanza kutoa tuzo hii. Tuzo italenga zaidi kutambua vyombo vya habari vyenye mtiririko mzuri wa kusaidia kuongeza wanawake katika nafasi za uongozi," alisema.

> **"Huu ni msimu wa nne tangu tulipoanza kutoa tuzo hii. Tuzo italenga zaidi kutambua vyombo vya habari vyenye mtiririko mzuri wa kusaidia kuongeza wanawake katika nafasi za uongozi," alisema.**

Alitaja vigezo kumpata mshindi wa tuzo hiyo ni kuwa na sera ya kijinsia, dawati la kijinsia, zana, tathmini na ufuatiliaji wa usawa wa kijinsia.

Nyingine ni idadi ya habari zilizoandikwa kuhusu wanawake na uongozi na nafasi ya wanawake waandishi wa habari katika chombo cha habari.

Alisema mradi wa kuwajengea uwezo wanawake kwenye uongozi (SWIL) uliwahi kuwapa mafunzo waandishi wa habari na kusaidia vyombo vya habari 11 kuandika na kufanya ufuatiliaji na tathmini katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2023.

"Tunaamini kuna vyombo vimeweza kuleta mabadiliko makubwa na vinahitaji kutambua na kuthaminiwa," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema dirisha la kupokea kazi liko wazi kuazia jana hadi Desemba 31, mwaka huu na zinazohitajika ni za kuanzia Januari.

Aliwataka waandishi wa habari kushiriki katika tuzo hiyo ili waweze kuibuka washindi na kuleta mabadiliko chanya katika jamii.




Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu tuzo za waandishi wa habari wanawake na uongozi zinazoandaliwa na chama hicho, zinazotarajiwa kutolewa Februari mwakani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Epukeni siasa za malumbano'

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ADA Tadea kimewataka wananchi kuachana na siasa zisizo na tija na kusisitiza kuwa Rais Dk. Hussein Mwinyi kuendelea kuongoza Zanzibar kwa kuwa anawajali na kuwaletea maendeleo.

Chama hicho kimesema malumbano yasio na msingi yamechangia visiwa vya Unguja na Pemba kusuasua kupata maendeleo na kujenga uchumi.

Mwenyekiti wa ADA Tadea, Juma Ali Khatib, aliyasema hao wakati akizungumzia nia ya serikali kutaka kuvunja nyumba chakavu na kujenga mpya.

Khatib, alisema uamuzi huo ni maendeleo yanayotakiwa na wananchi kuliko mivutano na misuguano ya kisiasa.

Alisema siasa zinazotakiwa ni za kujenga nchi na kustawisha maendeleo kiuchumi na kijamii.

"Siasa za kupigiwa makofi zimepitwa na wakati. Watu wanataka utumishi safi na maendeleo. Kuvunjwa nyumba kongwe na kujengwa mpya ni sehemu ya maendeleo," alisema Khatib.

Alisema madai ya chama chake tangu mwaka 1992 ni kupigania maendeleo, hivyo kimeridhishwa na juhudi za serikali hiyo inayoongozwa ma Rais Dk. Hussein Mwinyi kuwaletea wananchi maendeleo.

"Watawala walioko madarakani wailetee nchi maendeleo. Na sisi tunaotafuta kushika madaraka tukipate tulete maendeleo zaidi, malumbano kwenye majukwaa ya kisiasa yawe na wakati wake," alisema.

Khatib, alisema kwa ari, bidii na juhudi za Dk. Mwinyi, anatosha kupewa miaka mitano mingine amalizie kazi alioianza mwaka 2020.

# Vyama ushirika kupatiwa mikopo kuinuliwa kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaimarisha vyama vya ushirika na kutoa mikopo kwa wanachama wake ili kuwainua kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Khamis Suleiman Mwalim, wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya vyama hivyo visiwani hapa.

Mwalim, alisema kuwa sekta ya ushiriki ina umuhimu mkubwa kwa jamii na ni moja ya njia ya kujikwamua kiuchuni.

Alisema wakati umefika kwa wananchi kujiunga na vyama hivyo ili wanufaike na mikopo inayotolewa na kuondokana na umaskini wa kipato uliokithiri miongoni mwao.

Mwalim, alisema katika kufikia malengo ya vyama hivyo ni wajibu kwa waandishi hao kutumia kalamu zao na kuwa mabalozi kuielimisha wananchi kujiunga navyo. Akitoa mada katika mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika, Khamis Daud Simba, alisema ili kuwa na chama hicho imara, ni lazima viongozi kuheshimu maamuzi ya wanachama hasa kupitia mikutano yao mikuu.

Simba, aliwataka viongozi na wanachama wa vyama hivyo kufuata misingi ya ushirika, uwazi, uwajibikaji na kuijali jamii.

Alisema licha ya mafanikio iliyopata idara hiyo kwa kupata idadi kubwa ya vikundi vya ushirika, inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi, vitendea kazi na uelewa mdogo kwa jamii juu ya vyama hivyo.

Ofisa wa Maendeleo ya Vyama hivyo Zanzibar, Zainab Abulkadir, alisema maofisa ushirika wa wilaya wanafanya ukaguzi kila baada ya miezi mitatu ya wanachama, fedha, mikopo na mafunzo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 166 LA 2023**
**FLORENCE MWAIHOJO........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. **HERITAGE PROPERTIES LTD**
2. **ADILI AUCTION MART**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **HERITAGE PROPERTIES LTD**
2. **ADILI AUCTION MART**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**FLORENCE MWAIHOJO** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni Mwananyamala ). Shauri husika limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 12/11/24 saa 03:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W Sillas Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri w a Baraza hili leo tarehe 04 Mwezi 11,2024

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ABDULAZIZ MOHAMMED KHAMIS**

Anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki yenye namba za usajili **MC 478 AXV,MC 589BAT,MC 939CNF,MC 259CAB,MC 646CEX,MC 556CQC**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

Polisi Taarifa :

**PHQ/ DAR/KIN/243656/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MICHAEL KENNETH PHILLIPS**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDROVER** yenye namba ya usajili **T706 ADN.**

Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

**TAARIFA YA POLISI**

**PHQ/ARU/ARU/42689/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 27564 OF 2024**
**IN THE MATTERR OF THE ESTATE OF THE LATE**
**REV CHARLES SAMWELI MHANUSI**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APLICATION FOR**
**LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY PIUS JOSEPH ZUNGU**

**GENERAL CITATION**

**(Rules 75 of probte Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named desceased are hereby cites to come and see the proceedings if they think fit before the grant of lettters of Administration is made to the named petitioner. Objections to the grant should be field on or before the 02TH day of December 2024.
Dated at Korogwe this day of November 2024.

.............................................................

**RESIDENT MAGISTRATE**

**JAMHURI YA MUUNGANIO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katoka Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya SIHA**
**Kituo cha SANYA JUU Mkoa wa KILIMANJARO**
**Shauri la Mirathi Na. 35 /2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**TUMAINI AITAKU MAIMU W A WANDRI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTAMBUA MSIMAMIZI WA**
**MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA**
**RODRICK AFAELI MAIMU**

.........................................

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 11 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji kuteuliwa kuwa mwamuzi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuleta Mahakani kukaguliwa.
- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 10 mwaka 2024

.....................................

**HAKIMU**
**HAKMU MKAZI**
**MAHAKMA YA MWANZO**
**SANYA JUU**


**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 166 LA 2023**
**FLORENCE MWAIHOJO........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. **HERITAGE PROPERTIES LTD**
2. **ADILI AUCTION MART**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **HERITAGE PROPERTIES LTD**
2. **ADILI AUCTION MART**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**FLORENCE MWAIHOJO** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni Mwananyamala ). Shauri husika limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 12/11/24 saa 03:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W Sillas Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri w a Baraza hili leo tarehe 04 Mwezi 11,2024


**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 102 LA 2021**
**EMMA JIONATHAN MHAGAMA**
**MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. **ELIZA MATHEW SHIRIMA**
2. **PATRICK AMON MADA**
3. **JOSEPH KOMBA**
4. **THERESIA AKIDA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **ELIZA MATHEW SHIRIMA**
2. **PATRICK AMON MADA**
3. **JOSEPH KOMBA**
4. **THERESIA AKIDA**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**EMMANUEL JONATHAN MGAHAMA** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni Mwananyamala ). Shauri husika limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 20/11/24 saa 03:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W Sillas Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri w a Baraza hili leo tarehe 05 Mwezi 11,2024

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI**


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waafrika matumbo joto ushindi wa Donald Trump

Na Moshi Lusonzo


Rais mteule wa Marekani, Donald Trump. **PICHA: MTANDAO**

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, anasubiri kuingia Ikulu ya Marekani ya White House, baada ya kupata ushindi mnono katika uchaguzi mkuu uliofanyika Jumanne ya wiki hii.

Trump alimshinda Kamala Harris mgombea wa Democrat kwa kupata kura za kutosha za wajumbe maalum 294, ambao ni 24 ya wajumbe 270 wanaotakiwa kupata ushindi.

Trump alishinda majimbo muhimu kama Pennsylvania, Georgia, North Carolina na Wisconsin. Wafuasi wake wanamchukulia rais huyo mteule kutoka chama cha Republican kama mwokozi na shujaa, aliyekuwa tayari kutetea maadili yao dhidi ya wanamageuzi nchini Marekani.

Hata hivyo, wakosoaji wake ambao wanamwona kama kiongozi asiye na maadili, wanaeleza kushtushwa kwao kutokana na siasa zake kali, mienendo isiyo ya kiserikali, na matumizi yaliopindukia ya mitandao ya kijamii ndani na nje ya ofisi.

Watu waliokuwa na wasiwasi baada ya ushindi wa Donald Trump ni wahamiaji kutoka mataifa mbalimbali waliokwenda kutafuta maisha mazuri na hasa Waafrika.

### KIPINDI CHA HOFU

Baada ya Trump kuibuka kidedea, wahamiaji wengi wasio na vibali wameanza kupata hofu kutokana na ahadi ya kiongozi huyo kuwaondoa kinguvu nchini humo.

Hata hivyo, wana muda mdogo wa kukamilisha taratibu za kuishi nchini humo ikiwamo kupata vibali vya kuishi, kutokana na uongozi mpya utaanza kazi ndani ya miezi miwili ijayo.

Kulingana na Shirika la habari la Uingereza (BBC), baadhi ya Waafrika wameanza kufikiria kurudi kwenye mataifa yao kwa hiyari kabla ya zoezi la kuwaondoa kwa nguvu halijaanza pale Trump atakapoingia Ikulu.

Katika moja ya kampeni yake, Donald Trump alitoa kauli yenye utata akiwataja wahamiaji wa Haiti walioko eneo la Springfield, katika jimbo la Ohio, kama wezi wa paka na mbwa wa majirani zao na kuwafanya kitoweo.

Hata hivyo, madai hayo yalithibitishwa kuwa ya uwongo.

Wingi wa wahamiaji hawataki kungoja wakati wa muhula wa pili wa Trump ambao hautabiriki, wanaona kuangalia nyuma kwenye muhula wake wa kwanza kunaweza kutoa maarifa fulani kuhusu kitakachokuja.

### WASIWASI WA AFRIKA

Kwa viongozi wa mataifa ya Afrika, licha ya kumpongeza Trump kwa ushindi alioupata, wamekuwa na wasiwasi na uongozi wake baada ya kutambua hakutakuwa na usalama katika uongozi wake.

Viongozi wengi ambao wanaiona Marekani kama mshirika mkuu wa kutoa misaada ya kiuchumi na kijeshi, sasa kunaashiria mwanzo wa mtikisiko mkubwa.

Kiongozi huyo mwenye mtazamo wa kizalendo anatarajiwa kuongoza nchi hiyo tena kwa kipindi cha miaka minne, ambapo atakuwa karibu na washirika wake wa kisiasa na kupambana na maadui wa ndani na nje. Ingawa Trump anaweza kuwa na mipango mahsusi ya kukuza maslahi ya Marekani, historia yake inaonyesha kwamba bara la Afrika haliweki kipaumbele.

Ushindi huo wa Trump dhidi ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris ambaye alionekana mwenye mapenzi na Afrika, umepokelewa kwa shingo upande na viongozi barani Afrika.

Hata kwenye salamu zao za pongezi viongozi wa Afrika wameonyesha kuwa na hisia tofauti, kuna walionyesha matumaini kwa kuuzungumzia uongozi wake madhubuti, na wengine wakiwa na mashaka kuhusu namna ushindi huo utakavyoleta mustakabali wa bara hilo.

### MKATABA WA AGOA

Baadhi ya wachambuzi wa kiasiasa, wanasema hakuna uwezekano wa Trump kuongeza muda wa Ukuaji na Fursa za Kibiashara Afrika (AGOA) ambao unafikia tamati mwaka ujao.

Mkataba huo ambao ni muhimu kibiashara na kipaumbele kwa bara hilo, umekuwa na hofu ya kutoendelea, kuna ingawa wabunge wa chama chake cha Republican wanaunga mkono kuidhinishwa tena.

Katika mkataba huo unaziruhusu nchi za Afrika kusafirisha bidhaa zao Marekani bila kutozwa ushuru.

Prasan Nundlal, ambaye ni raia wa Afrika Kusini, anaelezea wasiwasi wake kuhusu Trump hasa linapokuja suala la mikataba ya kibiashara.

"Nina wasiwasi kuhusu mambo kama mikataba yetu ya kibiashara na Marekani kukataliwa, au kufungwa kwa sababu ya Donald Trump," alisema Nundlal.

Nundlal anaeleza anakisia kuwa utawala wa Trump utachukua mtazamo wa kimaadili na kivitendo akiweka kipaumbele kwa nchi yake pekee kama alivyokuwa akijinadi katika kampeni zake.

Hata hivyo, wachambuzi wanabainisha kuwa hali ya kutofuatiana ya mtazamo wa Marekani, inategemea kulingana na upande gani unaoshinda urais.

### KUKATA MISAADA

Afrika inapata misaada yake mingi kutoka Marekani, ambayo kwa mwaka huu pekee dola bilioni 3.7 ilitoa kwa nchi za Afrika kama msaada.

Lakini katika utawala wake wa Trump, alipendekeza kupunguza misaada ya kigeni duniani kote, hayo ni kulingana na ripoti ya Congress.

Hata hivyo, pendekezo hilo lilikataliwa na wabunge wa pande zote mbili.

Baraza la mahusiano ya Kigeni na Taasisi ya Ushaure ya Marekani ilisema kama upunguzaji huo ungetekelezwa, sera za jadi za Marekani kuhusiana na afya, ukuzaji wa demokrasia, na usaidizi wa usalama barani Afrika zingefutwa.

Kunaweza kuwa na msukumo mdogo wa kupunguzwa kwa misaada baada ya chama cha Republican kushinda viti vingi Bunge la Seneti na Baraza la Wawakilishi.

Pia kuna wasiwasi kwamba Trump anaweza kufunga mpango wa Pepfar, ambao umetumika muda mrefu na pesa nyingi katika kupambana na VVU barani Afrika.

> Ingawa muundo wa usalama wa taifa nchini Marekani unaiona Russia kuwa tishio, Trump binafsi hajaonekana kwamba anaona nchi hiyo kuwa tishio.

### WAHAMIAJI KUTOKA AFRIKA

Msimamo wa Trump kuhusu uhamiaji haramu uko wazi, wakati wa kampeni yake aliahidi kuwafukuza watu milioni moja ambao hawana vibali vya kisheria kuishi nchini Marekani.

Mnamo 2022, karibu wahamiaji 13,000 wa Kiafrika walisajiliwa kwenye mpaka wa Marekani na Mexico, kulingana na data ya Forodha ya Marekani na Ulinzi wa Mipaka.

Kufikia 2023, idadi iliongezeka na kufikia 58,000, huku baadhi ya wahamiaji wakitoa sababu ya kukimbia vita, mateso na umaskini.

Katika muhula wake wa kwanza, Trump alianzisha hatua zilizowazuia wahamiaji kutoka nchi kadhaa za Afrika, zikiwamo Nigeria, Eritrea, Sudan na Tanzania.

Tovuti ya habari ya Kenya ya Taifa Leo, iliripoti kwamba wahamiaji kutoka nchi hiyo wanaofikia 160,000, wana wasiwasi kwamba watakabiliwa uondoshwaji wa nguvu pale Trump atakapoapishwa kuwa rais.

### USALAMA NA MIGOGORO

Wakati Trump amekuwa nje ya madaraka kwa kipindi cha miaka minne, Russia imeongeza ushawishi wake kwa bara la Afrika.

Mojawapo ya njia kuu ambayo imefanya hivyo ni kwa kutoa wanajeshi na silaha kwa nchi zilizokumbwa na wanamgambo wa kijihadi, kama vile Mali, Niger na Burkina Faso.

Msimamo wa Russia umeitia wasiwasi Marekani na kuibua ushindani kati ya wapinzani hao wawili.

"Ingawa muundo wa usalama wa taifa nchini Marekani unaiona Russia kuwa tishio, Trump binafsi hajaonekana kwamba anaona nchi hiyo kuwa tishio," Moore aliambia BBC.

Kwa upande wa Nigeria, ujio wa Trump kwao ni kama furaha kwani wakati nchi hiyo ikipambana na kundi la Boko Haram, Trump ndiye aliidhinisha ununuzi wa ndege za Tucano.

Mbunge wa zamani nchini humo, Ehiozuwa Agbonayinmma, aliambia chombo cha habari cha Nigeria Vanguard kwamba ununuzi huo awali ulikataliwa na aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Barack Obama.

# MALINDI SC YAWAZA POINTI 18, MLANDEGE, KIPANGA ZANG'ARA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI timu yake inatarajia kukutana na Mafunzo katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau B, Kocha Mkuu wa Malindi SC, Ali Vuai Shein, amesema malengo yao ni kupata ushindi katika michezo sita iliyobakia ya mzunguko wa kwanza.

Wekundu hao wa Mji Mkongwe wanashuka uwanjani wakiwa na pointi 16 na wapo katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha jumla ya timu 16.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shein alisema wamejipanga kukabiliana ushindani katika mchezo huo na wamejipanga kuhakikisha hawapotezi pointi.

**Shein alisema kikosi chake tayari kimekamilisha maandalizi kuelekea mchezo huo ambao anaamini utakuwa mgumu kutokana na ubora walionyesha wapinzani wao katika michezo iliyopita.**

Aliongeza katika mchezo huo wachezaji wao wote wa kikosi cha kwanza watakuwa uwanjani kwa lengo moja la kusaka ushindi.

"Wako wachezaji wachache wenye majeraha ya kawaida lakini hawatakuwa sehemu ya kikosi hicho.

Tunataka kuhakikisha hatuondoki katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa ligi, ili kutimiza ndoto yetu hii inatupasa tushinde michezo iliyobakia katika huu mzunguko wa kwanza," Shein alisema.

Hata hivyo alisema anawaheshimu wapinzani wao kwa sababu wamekuwa ni moja ya timu ambazo zinafanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, lakini kikosi chao kinaundwa na wachezaji wengi wenye uzoefu na ligi hiyo.

Wakati huo huo Mlandege imepata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mwenge FC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Finya Arena ulioko Pemba, juzi jioni. Mabao ya Mlandege katika mechi hiyo yalifungwa na Mahmoud Mkonga, Abdallah Pinna na Aimar Hafidh.

Kwa matokeo hayo Mlandege imefikisha pointi 20 na kujiweka kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar sawa na Mafunzo ambao wana mchezo mmoja mkononi.

Wakati Mlandege akishinda michezo miwili mfululizo Wanajeshi wa Kipanga wao wamepata ushindi wa tatu mfululizo.

Mechi nyingine iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi ilimalizika kwa Kipanga kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Inter Zanzibar.

BZL imepata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Sharp Boys katika Ligi Daraja la Kwanza Unguja huku Ujamaa ikiwachapa Sebleni magoli 3-0 na Polisi ikiwafunga Ngome magoli 2-0.



Wachezaji wa Mlandege wakishangilia baada ya kupata bao katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya wenyeji Mwenge FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Finya, Pemba juzi jioni. Mlandege ilipata ushindi wa mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Simba Queens yaita mashabiki*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kurejea salama jijini Dar es Salaam, Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Sophia Mwasikili, amewaomba mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mechi dhidi ya watani zao, Yanga Princess, imeelezwa.

Yanga Princess itaikaribisha Simba Queens katika mechi ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa Novemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Mwasikili aliliambia gazeti hili jana kikosi chake kimeshaanza mazoezi kwa ajili ya mchezo huo ambao kwao wataingia uwanjani kwa leo la kulipa kisasi.

Beki na nahodha wa zamani wa Twiga Stars, alisema wamejiandaa kuonyesha ubora wao na kuwafuta 'machozi' mashabiki wao baada ya kupoteza mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya watani zao.

"Tunawaomba mashabiki wetu waje kwa wingi kutushangilia, tumejiandaa na tumejipanga kuwapa furaha, tunataka kuendelea mazuri, hatujapoa," Mwasikili alisema.

Simba Queens ndio vinara wa ligi hiyo wakishinda mechi zote tatu walizocheza wakifuatiwa na JKT Queens yenye pointi saba wakati Yanga Princess ina pointi tatu baada ya kutoka sare michezo yote waliyocheza.

## Wachezaji majeruhi JKT waanza kujinoa

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI waliojeruhiwa katika ajali ya basi la timu ya JKT Tanzania iliyotokea jijini Dar es Salaam Oktoba 27, mwaka huu, wameanza mazoezi mapesi chini ya uangalizi wa madaktari.

Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, alisema jana wachezaji wao wanaendelea vizuri na tayari wameanza mazoezi ili kujiandaa na michezo inayofuata ya Ligi Kuu Bara.

"Wachezaji wetu wanaendelea vizuri, bado wanaendelea kuwa chini ya uangalizi wa madaktari, lakini tayari wameanza kufanya mazoezi mepesi. Lengo warejee katika afya zao za kawaida na ya kimichezo ili wawe tayari kwa ajili ya michezo ijayo ya Ligi Kuu.

Hivi ninavyozungumza timu ipo kambini ikiwa na wachezaji wote walionusurika kwenye ajali pamoja na waliopata majeraha, tunashukuru hakuna mchezaji aliyepata majeraha makubwa kiasi cha kuhatarisha afya au karia yake ya soka, badala yale wameendelea kuwa fiti siku hadi siku," alisema Masau.

Aliongeza anaamini hadi kufikia Novemba 23, mwaka huu, wakati timu hiyo itakapocheza dhidi ya Prisons, nyota hao watakuwa tayari wamesharudi kwenye utimamu wa mwili wa kucheza mchezo huo.

"Kwa mujibu wa ratiba tutacheza na Prisons Novemba 24, nyumbani kwetu, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, mpaka muda huo tunaamini watakuwa wameshafanya mazoezi ya kutosha na kuimarika ili kukabiliana na ugumu na uzito na ushindani wa mechi hiyo," Bwire alisema.

Kikosi cha JKT Tanzania kikitokea Dodoma kilipata ajali maeneo ya Mbweni na kusababisha wachezaji 11 kujeruhiwa.

Wachezaji waliojeruhiwa baada ya basi hilo kupinduka ni nahodha, John Bocco, Danny Lyanga, Salum Gado, Gamba Matiko, Said Ndemla, Yacoub Selemani, Hassan Dilunga, Maka Edward, Hassan Mapalata, Hassan Machezo na Mohamed Bakari.

Kufuatia ajali hiyo, Bodi ya Ligi iliahirisha mchezo wao dhidi ya Simba uliokuwa uchezwe Oktoba 29, mwaka huu pamoja na mechi dhidi ya Namungo iliyokuwa ichezwe Novemba 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMWAZA TRENT

REAL Madrid inavutiwa sana na beki wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Trent Alexander-Arnold, 26, wanapojiandaa kuimarisha safu yao ya ulinzi. ***(AS)***

### MBEUMO ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE United imemjumuisha winga wa Cameroon, Bryan Mbeumo, 25, kwenye orodha ya wachezaji wanaowataka, huku Brentford ikiweka bei ya pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### KUDUS ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inataka kumnunua winga wa West Ham na Timu ya Taifa ya Ghana, Mohammed Kudus, 24, kama mbadala wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard (29), ambaye anawaniwa na klabu ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia. ***(Mirror)***

### DIAKITE KUMRITHI MATETA

MSHAMBULIAJI wa Reims kutoka Ivory Coast, Oumar Diakite, 20, atakuwa kipaumbele cha Crystal Palace ikiwa mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wao Mfaransa, Jean-Philippe Mateta (27), yatagonga mwamba. ***(Sun)***

### DORGU AGOMBEWA ENGLAND

MANCHESTER United na Chelsea zimeungana na Tottenham Hotspur katika mbio za kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Denmark, Patrick Dorgu, 20, ambaye kwa sasa anaichezea Lecce. ***(Football Insider)***

### O'BRIEN KUTUA MAREKANI

KIUNGO wa kati wa England, Lewis O'Brien, 26, anatarajiwa kuhamia Los Angeles FC kwa dau la pauni milioni saba wakati mkopo wake kutoka Nottingham Forest utakapokamilika ifikapo Januari. ***(Sun)***

### LOPETEGUI HALI TETE

KOCHA wa West Ham, Julen Lopetegui, anakabiliwa na shinikizo kubwa la kuondoka mapema baada ya kufahamishwa na uongozi wa klabu hiyo matokeo lazima yaboreshwe. ***(Times)***

### KOLO AGOMBEWA ULAYA

PARIS St-Germain na Randal Kolo Muani, 25, wako tayari kwa mchakato wa uhamisho wa mkopo ifikapo Januari, wakiwa pia na chaguo la kumnunua, huku baadhi ya klabu za Ligi Kuu England tayari zimewasilisha maombi ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Ufaransa. ***(Sky Sport Germany)***


### BARCA YAMTAKA LEAO

BARCELONA inafuatilia hali ya Rafael Leao, 25, katika klabu ya AC Milan iwapo winga huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno atapatikana. ***(Mundo Deportivo)***

### MADRID: VINICIUS HAELEWEKI

REAL Madrid imeanza kutilia shaka dhamira ya Vinicius Jr katika klabu hiyo na wana wasiwasi atafikiria kuondoka, huku Al-Hilal wakionyesha nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 24. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR KUTIBIWA WIKI NNE HADI SITA

**RIYADH,** Saudi Arabia

## Kuna tetesi huenda Al Hilal isimpe mkataba...

NEYMAR anatarajiwa kufanyiwa matibabu kwa muda wa wiki nne hadi sita baada ya kupata jeraha la misuli ya paja, Al Hilal imethibitisha, na kuzidisha uvumi juu ya mustakabali wa Mbrazil huyo na klabu hiyo ya Saudi Arabia.

**Neymar alicheza kwa mara ya pili katika klabu yake baada ya kuwa nje ya dimba kwa miezi 12.**

Aliingia kama mchezaji wa akiba katika dakika ya 58 ya ushindi wa mabao 3-0 ambao Al Hilal waliupata dhidi ya Esteghlal ya Iran kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa ya Asia iliyochezwa mapema wiki hii.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona aliinua mkono juu baada ya kupiga mpira ikiwa zimesalia dakika tatu na ikabidi abadilishwe.

"Kwa bahati mbaya, sio jeraha rahisi na anaonekana ana maumivu ya misuli na sio suala la goti," alisema Kocha wa Al Hilal, Jorge Jesus, katika mkutano na waandishi wa habari.

Neymar aliingia katika mitandao ya kijamii ili kuwaelezea mashabiki wake.

"Nina matumaini kurejea haraka," aliandika.

"Ni kawaida baada ya mwaka mmoja kuwa nje madaktari walikuwa tayari wamenionya, kwa hivyo lazima niwe mwangalifu na kucheza dakika zaidi."

Vyombo vya habari vya Saudi Arabia vilikisia Al Hilal huenda wasimwongezee mkataba Neymar, ambaye mkataba wake utamalizika Juni, 2025, kwa kipindi cha pili cha msimu wa Saudi Pro League.

Neymar amecheza mechi saba pekee kwa mabingwa hao mara 19 wa Saudia tangu asajiliwe Agosti mwaka, 2023 kwa ada iliyoripotiwa ya dola milioni 90.

Kwa sasa hajasajiliwa kucheza michezo ya ligi ya ndani kwa sababu klabu hiyo ina kikosi kamili cha wachezaji 10 wa kigeni, lakini anaruhusiwa kucheza mashindano ya bara.

Dirisha jipya la usajili linafunguliwa Januari 2025.

# ARTETA ALIA ARSENAL KUNYIMWA PENALTI




**MILAN,** Italia

MIKEL Arteta alionyesha hasira yake kwa kunyimwa "penalti ya asilimia 1,000" na kusisitiza Arsenal walifanya vyema zaidi Ulaya kwa miaka mingi licha ya kupoteza 1-0 dhidi ya Inter Milan.

Penalti ya Hakan Çalhanoglu katika muda wa dakika za lala salama ilisuluhisha mchuano mkali kwenye Uwanja wa San Siro na kuwapa washika bunduki hao kipigo kipya katika kampeni zao za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mikel Merino alihukumiwa alicheza faulo kwenye eneo la hatari dakika 17 baada ya kuhusika katika tukio upande wa pili wa uwanja ambapo alichezewa faulo na kipa wa Inter, Yann Sommer.

"Sielewi uamuzi huu," alisema Arteta.

"Hakuna hatari hata kidogo. Huwezi kujibu kwa sababu mpira uko karibu sana. Lakini sawa. Wanaamua hiyo ni penalti.

"Lakini ikiwa hiyo ni penalti basi ile ya Mikel Merino ambapo anampiga kichwani inabidi iwe penalti kwa asilimia 1,000. Hawa ndio washindi katika mchezo huu na ni vigumu sana kukubali.

"Tuliambiwa mwanzoni mwa msimu hiyo haikuwa penalti. Hiyo ilikuwa wazi. Leo ilikuwa hadithi tofauti."

Baada ya kuanza polepole ambapo Denzel Dumfries aligonga mwamba wa goli katika dakika ya pili, Arsenal walizidi kumiliki mpira lakini hawakutafuta njia ya kumfunga, Sommer.

Matokeo hayo yanaifanya Arsenal kushika nafasi ya 12 katika jedwali la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Bayern waomboleza kifo cha shabiki wao




**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich inaomboleza kifo cha shabiki wao aliyehudhuria ushindi wa bao 1-0 wa timu hiyo dhidi ya Benfica kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi usiku.

Klabu hiyo ya Bavaria ilisema mapema jana asubuhi walipokea habari shabiki wa timu yao alifariki wakati akisafirishwa kupelekwa hospitali.

Mashabiki wa Bayern hawakuimba wakati wa mchezo kwa heshima ya shabiki huyo.

Hali kwenye Uwanja wa Bayern Munich ilinyamazishwa kwa kiasi kikubwa dakika chache baada ya mchezo kuanza ilipobainika kulikuwa na dharura ya kiafya iliyohitaji uangalizi wa wahudumu wa afya na maofisa wa polisi.

Kundi la mashabiki wa Bayern Club Nr. 12 ilisema wanachama wake "hawatashangilia kama kawaida kwa sababu ya uingiliaji wa dharura wa matibabu. Maisha huja kabla ya mchezo. Tunawatakia familia na marafiki nguvu nyingi."

Mashabiki wa Bayern hawakuanza tena kuimba baada ya mtu huyo kutolewa nje ya uwanja kwa machela baada ya takriban nusu saa.

"Dharura ya kiafya katika viwanja vya Allianz Arena iliweka kivuli kwenye mchezo tangu mwanzo," ilisema taarifa ya Bayern.

"Kwa kuzingatia, Südkurve ilijiepusha na uungwaji mkono wake wa kawaida kwa timu yao, na klabu pia ilipunguza utangazaji wake wa mechi."

Bao la kichwa la Jamal Musiala dakika ya 67 lilitosha kwa Bayern kumaliza mwendo wake wa kupoteza michezo miwili na kupata ushindi wake wa pili wa michuano hiyo.

Mashabiki wa Bayern walishangilia bao hilo, lakini hali ilibaki kimya kwa muda wote wa mechi.

# Barca wao wanachapa yeyote

**BELGRADE,** Serbia

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, anataka timu yake kuendeleza msururu wa kufunga mabao baada ya kuwalaza Red Star Belgrade magoli 5-2 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku na kuendeleza mbio zao za ushindi hadi michezo saba katika mashindano yote.

Barca wamefunga angalau mara tatu katika kila moja ya ushindi huo saba -- ikijumuisha michezo minne dhidi ya Bayern Munich na Real Madrid -- na wamefunga mabao matatu au zaidi katika mechi 10 kati ya 16 msimu huu.

Katika LaLiga na Ligi ya Mabingwa, tayari wameshafunga mabao 55, wastani wa zaidi ya 3.4 kwa kila mchezo, na Flick anasema mapenzi ya wachezaji kwa ajili ya mashindano ndiyo yanawasukuma.


"Maonyesho ni mazuri sana," alisema Flick katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo.

"Ninaifurahia sana timu na nadhani matokeo, wanazungumza lugha yao wenyewe.

"Tunachofanya, kwa umakini katika kila mechi, unaweza kukiona. Wachezaji wanafanya vizuri kuhusu mpango wa mechi tulionao. Wanatambua uwanjani na hii ni nzuri kuona.

"Natumaini tunaweza kudumisha, kwa hakika tuna imani. Sio tu kwa sababu ya mechi hii, lakini kwa sababu ya msimu mzima ambao tumecheza hadi sasa.

"Timu inafanya vizuri kwa sababu wanapenda kucheza mpira na wanapenda kushindana na timu yoyote, bora zaidi wanapenda kushindana na kila timu. Tunataka kuwa na muda katika kiwango hiki na tunafanya kazi ngumu kwa hilo."



## Gamondi apata dawa wanaopaki

INATOKA UK. 24

"Kucheza michezo mingi kwa muda mfupi pia kunasababisha wachezaji wangu kushindwa kuonyesha viwango vyao vilivyozoeleka kwa mashabiki. Tunacheza mechi kila baada ya siku tatu, na hii sisemi kwa wachezaji wangu tu, hata kwa timu nyingine wakati mwingine tunakwenda kucheza mchezo bila maandalizi baada ya kucheza uliopita," alifafanua.

Ingawa Yanga haijapata ushindi wa idadi kubwa ya mabao kama ilivyokuwa msimu uliopita, ukiacha ule wa mabao 4-0 dhidi ya Pamba Jiji, lakini timu hiyo imeweka rekodi ya kucheza michezo nane bila kupoteza.

Mabingwa hao watetezi waliruhusu rekodi yao kutibuliwa Jumamosi iliyopita walipofungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC.

Msimu uliopita ambao Yanga ilikuwa ikifunga mabao mengi, ilipoteza mchezo katika mechi ya nne tu baada ya kuanza kwa ligi ambapo Oktoba 4, mwaka jana ikiwa Mbarali, Mbeya nyumbani kwa Ihefu FC ililala mabao 2-1.

## Fadlu afichua ya moyoni

INATOKA UK. 24

sijakipata, hili nalifanyia kazi kwa sababu kuna wakati tunakuwa katika ubora unaotakiwa, lakini baadaye tunashuka, mchezo mmoja tunakuwa na kasi tofauti, tunapanda na kushuka, hili ni tatizo, nadhani tukicheza kwa kasi kwa dakika zote 90, Simba itakuwa hatari sana," Fadlu aliongeza.

Kuhusu kutoa nafasi kwa wachezaji wote, Fadlu alisema kikosi chake kimekuwa na ushindani wa namba kwa sababu anatoa nafasi kwa kila mchezaji kuitumikia timu hiyo.

"Nataka kila mmoja acheze, timu ikishinda ishinde kama timu, sitaki kikosi chenye kutegemea mchezaji mmoja au wachache ambao kama wakikosekana inakuwa katika hatari ya kupoteza mchezo," alisema.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, alisema makosa ya kizembe yaliyofanya na wachezaji wake yamesababisha timu yake kupokea kichapo hicho.

Moallin alisema walianza vyema mchezo huo lakini walipokuwa nyuma kwa mabao mawili, hali ilibadilika na wachezaji walianza kupoteza hali ya kujiamini.

# PRISONS YAJICHIMBIA DAR IKIIWINDA JKT TANZANIA

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya Prisons imesema mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa kuweka kambi yake jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na michezo ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha michezo ya kimataifa, huku wachezaji wengi wakitimkia katika vikosi vya timu zao za taifa vinavyosaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazofanyika mwakani nchini, Morocco.

Mtendaji Mkuu wa Prisons, John Matei, ameliambia gazeti hili kikosi cha timu hiyo kitaanza mazoezi yake rasmi kesho baada ya wachezaji kumaliza mapumziko ya siku sita.

**Matei alisema baada ya kuifunga KenGold bao 1-0 Jumapili iliyopita, waliamua kuwapa wachezaji wao mapumziko mafupi kwa sababu mechi yao inayofuata dhidi ya JKT Tanzania itachezwa Novemba 24, mwaka huu.**

"Baada ya kumaliza mechi ya KenGold tulivunja kambi na kuwapa vijana mapumziko ya kama wiki moja au siku sita hivi, Novemba 9 (kesho) wanatakiwa kurejea kambini kujiandaa na michezo ijayo, kambi yetu kama kila kitu kikienda sawa, tutayafanyia Dar es Salaam, na kipindi chote hiki cha mapumziko ya FIFA, sisi tutakuwa kambini," Matei alisema.

Matei alisema sababu kubwa ya kuweka kambi Dar es Salaam ni kuwa karibu na eneo ambalo mchezo wao dhidi ya JKT Tanzania utachezwa.

"Mchezo wetu wa kwanza baada ya mapumziko hayo ni dhidi ya JKT Tanzania utakaochezwa Dar es Salaam, na hiyo ndiyo sababu kubwa imesababisha tuwe huko karibu zaidi au sehemu hiyo hiyo ambayo tutacheza mchezo wetu wa Novemba 24," Matei aliongeza.

Prisons iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Mbwana Makata, ipo katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 10 kibindoni baada ya kucheza michezo 10, imeshinda miwili, sare nne na kupoteza mechi nne.

Kikosi cha JKT Tanzania nacho kinaendelea na mazoezi huku uongozi ukisema wachezaji wote walioumia katika ajali wanaendelea vyema na wameanza mazoezi mepesi chini ya uangalizi wa madaktari wa timu hiyo.




Golikipa wa Dodoma Jiji FC, Ngeleka Katumbua, akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazoendelea baada ya kumalizika kwa Kalenda ya Kimataifa. **PICHA: MTANDAO**

# *Kuogelea vijana kuchuana Burundi*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya vijana ya kuogelea itaondoka nchini Novemba 21, mwaka huu kuelekea Burundi ili kushiriki mashindano ya mchezo huo ya Kanda ya Tatu Afrika.

Mashindano hayo yanatarajia kufanyika Novemba 23 na 24, mwaka huu nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Michael Livingstone, alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana wenye umri kuanzia miaka 12 na kuendelea na Tanzania itawakilishwa na waogeleaji 41.

"Maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yanaendelea vizuri, kila klabu inajinoa na kwa upande wa wachezaji waliopo Dar es Salaam huwa wanafanya mazoezi asubuhi kwenye bwawa la kuogelea IST chini ya HPT, na jioni wanafanya kwenye mabwawa mengine, " alisema Livingstone.

Kocha huyo alisema mashindano hayo yatashirikisha waogeleaji kutoka klabu za Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar huku lengo lake ni kuwapa uzoefu wachezaji wa hapa nchini kuelekea michuano ya dunia.

"Tunaiomba serikali itusaidie kuziandaa timu za vijana ili ziwe zinapata mazoezi ya muda mrefu, mara nyingi wazazi huwa wanatumia gharama zao ili watoto wafanye mazoezi, endapo wakishindwa gharama hizo tunapoteza vipaji, " kocha huyo alisema.

# Michezo

Ijumaa Novemba 8, 2024

Nipashe





Neymar kutibiwa wiki 4 - 6 UKURASA 21



Mshambuliaji wa kimataifa wa Simba kutoka Uganda, Steven Mukwala (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Gamondi apata dawa wanaopaki 'bus' Bara

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema timu nyingi za Ligi Kuu Tanzania Bara zimekuwa na utamaduni wa 'kupaki basi' kila wanapocheza nazo na kuiweka timu yake katika nafasi ngumu ya kufunga idadi kubwa ya mabao.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kushuka dimbani kuivaa Tabora United jana jioni, Gamondi alisema mafanikio waliyopata katika misimu miwili iliyopita yamewafanya wapinzani wacheze kwa tahadhari na yeye tayari amejifunza 'kitu' na amepata dawa ya tatizo hilo.

Gamondi alisema bila kuficha Yanga ndiyo timu bora kwa sasa hapa Tanzania, hivyo timu nyingine zimekuwa zikicheza kwa tahadhari wanapokutana ili kujiepusha na kufungwa mabao mengi.

Alisema timu nyingi zimekuwa zikicheza mfumo wa kuweka idadi kubwa ya wachezaji nyuma kwa sababu zinajua kama zitafunguka, zinaweza kujikuta zinapokea dozi kubwa kama walivyofanya katika mechi nyingi msimu uliomalizika.

"Yanga ndiyo timu bora kwa sasa nchini, ndiyo maana kila timu ikija kucheza na sisi inakuja kwa tahadhari. Zinajua zikicheza na sisi kwa kupishana zitafungwa idadi kubwa ya mabao. Ni kazi sana kuzifungua timu kama hizi, kupiga krosi na kutafuta nafasi kwa ajili ya kufunga," Gamondi alisema.

Aliongeza hii ndiyo sababu inayofanya msimu huu wasiwe na idadi kubwa ya mabao, lakini ameahidi kuendelea kulifanyia kazi ili kurejea walipopazoea.

"Vitu vinavyotokea kwa sasa, tunapata mambo ya kujifunza, siku zote changamoto inakufanya ujue ufanye nini ili utatue tatizo, tunatakiwa turekebishe hili. Kinachobaki kila kitu ni upande wetu, tufanye nini kuwafungua wapinzani kwa kila staili tunayoweza hadi kushinda michezo yetu," alisema kocha huyo.

Aliongeza sababu nyingine inayowafanya wachezaji wake waonekane wamepungua viwango ni idadi kubwa ya mechi wanazocheza ndani ya muda mfupi.

INAENDELEA UKURASA 23

# Fadlu afichua ya moyoni

### Amekumbushia penalti walionyimwa Simba mechi...

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya KMC juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema anafurahia namna wachezaji wake wanavyopambana huku akigusia walinyimwa penalti katika mechi waliyopoteza dhidi ya watani zao Yanga iliyochezwa Oktoba 19, mwaka huu.

**Simba imefikisha pointi 25 baada ya kucheza michezo 10 ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, imeshinda mara nane, imetoka sare moja na imepoteza mechi moja.**

Fadlu alisema kwa sasa kila mchezaji anayepewa nafasi ya kuanza katika kikosi chake anafanya kile anachokitaka na inasaidia kupata matokeo mazuri.

"Nimefurahi namna timu ilivyocheza, muhimu pointi tatu na namna timu inavyocheza... tulistahili ushindi huu," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema wamekuwa wakipambana kucheza vizuri katika kila mchezo lakini baadhi ya vitu vinawanyima ushindi kwenye baadhi ya mechi.

"Tulicheza vizuri dhidi ya Yanga, maoni yangu nadhani tulistahili kupata penalti mbili kwa Kibu, lakini huwezi kuhoji maamuzi yaliyotolewa, tunaendelea na mbio zetu, nafurahi kuona timu inazidi kuimarika na tunapata matokeo," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa mawazo wanayaelekeza katika michezo iliyopo mbele huku wakizidi kukiimarisha kikosi chao.

"Tutakuwa na mapumziko mafupi kwa ajili ya kalenda ya mechi za kimataifa za timu za taifa, tutayatumia kujiimarisha zaidi kabla ya kurejea tena katika ligi," Fadlu aliongeza.

Kocha huyo aliongeza kama wachezaji wake wangekuwa na utulivu, wangepata mabao mengi zaidi katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye KMC Complex, hapa jijini.

Hata hivyo alisema bado kikosi chake hakichezi kwa kasi na ubora wa juu ndani ya dakika zote 90.

"Ninawapongeza vijana wangu kwa ushindi na kwa kuzingatia maelekezo yangu, lakini sijaridhika na idadi ndogo ya mabao kipindi cha kwanza. Tumepoteza mabao matatu kabla ya kupata goli la kwanza, nadhani ilitakiwa liwe la nne, kipindi cha pili wapinzani wakabadilika, baadaye tukauchukua mchezo na kufunga mawili mengine, dakika 10 za mwisho hatukuwa katika ubora wetu," kocha huyo raia wa Afrika Kusini, alisema.

Aliongeza kwa kushirikiana na wasaidizi wake wataendelea kuimarisha maeneo wanayofanya vizuri na kurekebisha pale ambapo bado wanaona hawachezi katika ubora anaoutaka.

"Bado kuna kitu nakitafuta na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >